

UKURASA 22

**KESI YA UZEMBE KIFO CHA MARADONA OKTOBA MOSI**


epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
IJumaa Mei 31, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581693
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Mbunge wa CCM ajichongea kwa kuomba uwaziri

• **Katibu** Mkuu awaka, amjibu hafai hata ubunge... *Ukurasa 5*



UKURASA WA 19

## JESHI LA ISRAEL LADHIBITI UKANDA WA PHILADELPH

JESHI la Israel (IDF) limesema kuwa limechukua udhibiti wa eneo la kimkakati kwenye mpaka kati ya...



## Polisi wafutwa kazi kwa matumizi mabaya 'tochi'



UKURASA 2



Mhariri Mtendaji wa Gazeti Nipashe, Beatrice Bandawe akionesha Tuzo ya Mwanamke Kiongozi katika Chombo cha Habari 2024, iliyotolewa na Umoja wa Wachapishaji wa Magazeti Duniani (WAN-IFRA), baada ya kukabidhiwa katika hafla iliyofanyika Copenhagen, Denmark mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 3

## LEMA: SINA MPANGO WA KUGOMBEA UONGOZI CHADEMA




MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema...

UKURASA WA 4

## BABA KIZIMBANI KWA MASHTAKA YA KUUA MWANAWE KISA 700/-



MKAZI wa Kijiji cha Chigunga, wilayani Geita, Stefano Mlenda (31), amepandishwa kizimbani...



UKURASA WA 17

## ZANZIBAR WALALAMA MIZIGO KUKAGULIWA NA MBWA BANDARINI

MWAKILISHI wa Mtabwe, Dk. Mohammed Ali Suleiman amesema kumekuwa na kadhia katika Bandari ya Dar es Salaam...

## TACAIDS: Wanaume wa umri miaka 50-54 hatari kwa VVU

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA SC YAANZA KUPITISHA PANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# TACAIDS: Wanaume wa umri miaka 50-54 hatari kwa VVU

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WANAUME wenye umri wa miaka 50-54 ndiyo kundi linaloongoza kwa ushamiri wa Virusi vya Ukimwi (VVU) nchini, Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) imebainisha.

Kwa upande wa wanawake, takwimu za TACAIDS zinaonesha kinamama wenye umri kuanzia miaka 45-49 wanaongoza kwa ushamiri wa VVU huku wasichana wenye umri wa kuanzia miaka 15-24 ndiyo kundi hatarishi zaidi kwa maambukizo mapya ya VVU kitaifa.

Dk. Jerome Kamwela, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, aliyasema hayo juzi mjini Morogoro katika wasilisho lake wakati wa semina kwa ajili ya wahariri na waandishi wa habari juu ya hali ya maambukizi ya VVU, unyanyapaa, Sheria ya Ukimwi na njia bora ya kutumia vyombo vya habari kutoa elimu sahihi ya kujikinga na VVU kwa vijana.

Akirejea utafiti wa Ukimwi (THIS 2022/23), Dk. Kamwela alisema Tanzania ina watu 1,548,000 wanaoishi na VVU (WAVIU).

Mkurugenzi huyo alisema kiwango cha maambukizi mpya kwa watu wazima wenye umri wa kuanzia miaka 15 kimepungua kwa asilimia 16.7 kutoka 72,000 (THIS 2016/17) hadi 60,000 (THIS 2022/23).

Hata hivyo, Dk. Kamwela alisema maambukizi mapya ya VVU yameongezeka maradufu katika kipindi tajwa kwa wasichana wenye umri wa miaka 15-24.

"Utafiti unaonesha maambukizi mapya yamepungua kwa wanaume wa rika zote (watoto na watu wazima) sawa na ilivyo kwa kundi la wanawake watu wazima wenye umri wa kuanzia miaka 15," alisema Dk. Kamwela na kuongeza:

"Ushamiri wa VVU kwa watu wazima (15+) ni wa asilimia 4.5, uko juu zaidi kwa wanawake (asilimia 5.6) kulinganishwa na wanaume (asilimia tatu)."

Dk. Kamwela alisema wastani wa ushamiri wa VVU ni wastani wa asilimia 1.7 mkoani Kigoma (kiwango cha chini) hadi asilimia 12.7 mkoani Njombe (kiwango cha juu zaidi).

Alitaja mikoa mitatu ya Njombe, Iringa na Mbeya kuwa juu ya wastani wa kitaifa wa ushamiri wa VVU wa asilimia tisa.

Kuhusu utekelezaji wa malengo ya "95-95-95" kufikia mwaka 2025, Dk. Kamwela alisema Tanzania imeshafanikiwa kufikia 95 ya pili kati ya tatu za malengo ya dunia.

95-95-95 zina maana kwamba "asilimia 95 ya WAVIU wawe wamejua hali zao za VVU, asilimia 95 ya WAVIU wanaojua wanaishi na VVU wawe wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU na asilimia 95 ya WAVIU wanaopata matibabu wawe wamepunguza makali ya VVU".

Dk. Kamwela alisema kuwa katika 95 ya kwanza, Tanzania bado iko chini. Kwa watu wazima utambuzi wa WAVIU uko kwa asilimia 78. Wanaume wako nyuma katika kupima afya zao. Vijana wako nyuma zaidi katika kupima kujua kama wana maambukizi.

## HALI YA VVU KITAIFA






**1,548,000**

**Idadi ya watu wanaoishi na VVU (WAVIU) nchini mwaka 2022/23.** CHANZO: THIS 2022/23

**15-24**

**Wasichana wa miaka 15-24 ndiyo kundi linaloongoza kwa kuambukizwa zaidi.**






**50-54**

**Kiwango cha ushamiri wa VVU kwa wanaume kiko juu zaidi kwa kundi la wenye umri wa miaka 50-54.**

**MIKOA MITATU**

**Mikoa yenye kiwango kikubwa cha ushamiri wa VVU ni Njombe, Iringa na Mbeya.**

Victoria Finance
Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | AISHA WAZIRI NTALA | NYUMBA | HALI MILIKI MALI YA ALLY R. NKANYANGA KITALU NA. P23603 ULONGONI (B) ILALA | LEHALEL GROUP | 14-06-2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

MASHARTI YA MNADA;
- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa kama ilivyo.

**SIRI MIKOA 3**

Wakati mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya ikinyooshewa kidole kuwa na kiwango kikubwa cha ushamiri wa VVU, Dk. Kamwela akaibuka na mtazamo tofauti.

Alisema kuwa Mkoa wa Njombe ambao una ushamiri wake wa VVU ni wa wastani wa asilimia 11.6 kwa wanaume na 12.7 (wanawake), katika 95 ya tatu (kupunguza makali ya VVU) una wastani wa asilimia 60.5 (wanaume) na asilimia 86.7 (wanawake).

Kwa Mkoa wa Iringa, Kaimu Mkurugenzi Kamwela aliutaja una ushamiri wa VVU kwa asilimia 11.2 (wanaume) na asilimia 11.1 (wanawake). Hali ya utekelezaji 95 ya tatu iko kwa asilimia 56.6 wanaume na asilimia 83.9 kwa wanawake.

Kwa mujibu wa Dk. Kamwela, ushamiri wa VVU mkoani Mbeya ni wa asilimia 9.2 (wanaume) na asilimia 9.6 (wanawake). Walifanikiwa kupunguza makali ya VVU ni asilimia 57.4 kwa wanaume na asilimia 83.2 kwa wanawake.

Ni takwimu zinazotoa ishara ya idadi ndogo ya WAVIU wanaofariki kutokana na Ukimwi, hivyo kuifanya mikoa hiyo kuonekana kuwa na idadi kubwa ya WAVIU.

**MFUKO WA UKIMWI**

Kaimu Mkurugenzi Kamwela pia alitoa rai kwa wadau kuchangia fedha kutunisha Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI badala ya kutegemea ufadhili kutoka nje ya nchi.

Alisema ripoti mpya ya Shirika la Afya Duniani ya mwaka huu inaonesha asilimia 60 ya WAVIU wako Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, shida kuu ikiwa ni hali duni kimaisha kwa wakazi wa eneo hilo.

"Ufadhili wa mataifa makubwa kiuchumi hivi sasa umeelekezwa kwenye miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Afrika tukubaliane kuwekeza fedha zetu za ndani kulinda watu wetu dhidi ya VVU/Ukimwi," alisema.

Kaimu Mkurugenzi huyo pia alitoa angalizo kwa wananchi kuwa kadri maeneo yao yanapokua kiuchumi au kupata miradi mipya maendeleo, ndivyo ongezeko la maambukizi ya VVU linavyowakumba.

Alisema utekelezaji miradi huenda sambamba na kuhamia kwa wageni kwenye eneo husika, akisisitiza "jamii inapopokea wageni, ijichunge".

"Mkoa wa Dodoma ulikuwa na kiwango kidogo cha maambukizi ya VVU, serikali ilipohamia Dodoma kiwango kimeongezeka.

"Tanga pia ilikuwa na idadi ndogo ya maambukizi, ilipopata miradi mikubwa ya kimkakati, ikiwamo bandari, sasa kuna ongezeko la maambukizi ya VVU," alisema.

HABARI KITAIFA



Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda (kulia), akisalimiana na Katibu wa Machifu wa Mikoa ya Mbeya na Songwe, Chifu Edward Mwanjali walipokutana katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Makonda akerwa utendaji Jiji Arusha

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, ameelezea kukerwa na utekelezaji duni wa miradi katika Halmashauri ya Jiji la Arusha licha ya kupatiwa Sh. bilioni 7.7 mwaka 2023/24 na kutumia Sh. milioni 500 pekee.

Amesema kutokana na utekelezaji huo hafifu, ingekuwa amri yake, angeifuta halmashauri hiyo.

Makonda aliyasema hao jana wakati akipokea ripoti ya miradi katika halmashauri hiyo huku akisema ni jambo la kushangaza serikali kuu imetoa fedha hizo lakini imetumia Sh. milioni 500 na miradi ikibaki bila kutekelezwa.

"Naibu Meya nimejiuliza kwa nini tuna jiji kama miradi yote hiyo ilitakiwa kutekelezwa alafu haijatekelezwa? Tumebakiza mwezi mmoja na fedha zipo. Akili yangu ya haraka haraka, ingekuwa ni mamlaka yangu ningewafukuza kazi wote.

"Si tu kuwafukuza kazi. Kule Marekani katiba inasema Rais anaweza kutoka madarakani kutokana na afya na mambo mengine. Hapa nawaza hakuna utaratibu unang'olewa kwenye majukumu yako kwa sababu umeshindwa kutimiza na kushtakiwa kupoteza muda wa wananchi," alisema.

Makonda alisema mamilioni ya fedha ambayo yapo na ukiangalia ripoti ya mwisho inaonyesha kuwa serikali kuu imeipatia halmashauri hiyo Sh. bilioni 7.75 na fedha iliyotumika ni Sh milioni 500.

Alisema Halmashauri zingine hazina fedha na zinahitaji fedha lakini Jiji Arusha imepatiwa na zilizotumika ni sawa na asilimia 6.4 tu.

Makonda pia alisema makusanyo ya halmashauri hiyo ni zaidi ya Sh. bilioni 30.5, fedha ilizotoa ni Sh. bilioni 17 kutoka kwenye makusanyo yake na zilizotumika ni Sh. bilioni 3.9.

"Kwa lugha nyingine, mnazo fedha mmezitoa huko mtaani sijui zinafanya nini na Sh. bilioni 14 hazijatumika katika mapato ya Sh. bilioni 30. Najiuliza hapa kuna watu wana akili timamu kweli? Nawaambia hii halmashauri tutawapiga spana mpaka mtanyooka. Mkurugenzi tutawapiga spana mpaka mtanyooka," alisema.

Makonda alisema haiwezekani wakawa na fedha zote hizo alafu wakienda katika miradi hakuna kilichofanyika.

"Ukisoma ripoti unaambiwa kuna Sh. bilioni 20 ambazo zitaenda kwa mwaka mwingine wa fedha kana kwamba kuna miradi iliyokamilika. Miradi haikamiliki wasambazaji wanadai fedha, hawalipwi na fedha mnazo mnaamua sasa mzipeleke mwaka ujao wa bajeti baadaye mje mseme mfumo haufanyi kazi?

"Ujue nawaza sijui watu wanapataje kazi. Najiuliza watu wanafanyaje mpaka wanaonekana wa maana jamani. Kama ushirikina upo, basi hii nchi inao. Tukipita katika miradi tutaona hata jengo lao la utawala sijui linaendaje. Sijui ni kitu gani kinaendelea mmepewa kazi ya kuwaletea wananchi maendeleo au ya kuonyesha nani mkubwa?"

"Ukiangalia utaona zabuni karudisha imetangazwa upya kwa mara ya pili, mradi haujaanza kutekelezwa. Idara ya elimu haijawasilisha mahitaji katika kitengo cha uanunuzi. Zabuni ilikosa mzabuni na kutangazwa kwa mara ya pili mara mradi haujaanza kutekelezwa elimu ya msingi haijawasilisha mahitaji katika kitengo cha ununuzi. Hivi ndivyo tunavyofanya kazi?" alihoji.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, alisema kuna changamoto ya miradi ya maendeleo kwa wananchi kutokukamilika kwa wakati.

"Hii ni changamoto kubwa katika jiji la Arusha na kama ukiangalia taarifa, kumekuwa na mivutano mingi kati ya baraza (la madiwani) na menejimenti na mheshimiwa mbunge kiasi kwamba inadhohofisha utoaji wa huduma katika miradi ya maendeleo," alisema.

Mtahengerwa alisema jambo hilo linawaathiri kwa kiwango kikubwa na akiwa kiongozi, amefanya jitihada za kuwaeleza japo bado kuna tatizo.

Alisema asilimia 18 ni aibu kumekuwa na migongano, malumbano na kutoelewana baina yao, hivyo kusababisha kuwaadhibu wananchi wasio na hatia na mbaya zaidi serikali imeshatoa fedha hizo.

"Inapofikia kwenye matumizi inakuwa changamoto. Utaangalia katika taarifa namna gani miradi imekuwa na sitofahamu licha ya fedha kutolewa na sababu ya pili halmashauri tunadaiwa na wazabuni na ukienda kwenye kikao, utasikia na hakuna sababu za msingi kuacha kuwalipa wanazungushwa wanapodai,"alisema.

Mtahengerwa alisema watu wanaichukia serikali kwa sababu kuna baadhi ya watu wamekalia viti hawataki kutimiza wajibu wao ipasavyo.

Alisema kuna watu wameuziwa nyumba na mali zao kutaifishwa kwa sababu ya uzembe wa viongozi kama nyaraka ya mtu ina changamoto anatakiwa kuambiwa akairekebishe ili apatiwe malipo jambo ambalo halifanyiki.

# Lema ajitoa uenyekiti Kanda ya Kaskazini

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, ametanagza kutogombea tena nafasi hiyo katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwaka huu.

Katika ukurasa wake wa X zamani twitter, Lema, Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, ametoa kauli hiyo ikiwa ni siku moja baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa kanda za Nyasa, Serengeti na Magharibi.

Kauli hiyo ya Lema, imezua mjadala kwenye mitandao ya kijamii kuhusu uamuzi wake ambao huku baadhi ya watu wakidai huenda amefanya hivyo kwa hasira baada ya rafiki yake, Mchungaji Peter Msigwa, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa, kubwagwa juzi kwenye uchaguzi wa kanda hiyo.

Msigwa alikuwa akichuana na Mbunge wa zamani wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi (Sugu), ambaye alimshinda kwa kura 54 dhidi ya 52 alizopata.

Katika ukurasa wake wa X, Lema aliandika: "Kwa ajili ya ustawi wa chama changu na uimara wake katika kujenga misingi bora na muhimu hasa katika kipindi hiki tunachoelekea katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji na uchaguzi mkuu 2025, sitagombea nafasi ya mwenyekiti wa kanda kwa mara hii katika uchaguzi unaokuja.

"Kwa sasa nitafanya wajibu wangu muhimu wa ujenzi wa chama katika kipindi kilichobaki.

Baada ya kumalizika kwa uchaguzi Kanda ya Nyasa na Sugu kutangazwa Mch. Msigwa, alizungumza na kumpongeza huku akisema ataendelea kuwa mwanachama na ataendelea kushiriki katika kukijenga.

Baada ya kauli hiyo ya Msigwa, Lema alimpongeza kwa kukubali matokeo.

"Hongera kwa mapambano na pole kwa uchaguzi. Nimefurahi niliposikia hotuba yako baada ya uchaguzi wa Kanda ya Nyasa kumalizika. Umesema "Thamani yako si cheo. What you actualy mean is 'leadership is not title. Fantasistic.

"Na pia muhimu zaidi umesisitiza kuendelea kuwa mwanachama senior (mwandamizi) wa chama na uko tayari kutumwa popote kutoa uzoefu na nguvu zako, jambo la baraka sana. Hutakuwa mpweke kwa muda mrefu sana katika klabu ya wanachama senior, watu wengi tutaungana na wewe katika siku za hivi karibuni, pengine kwa style tofauti tu," aliandika Lema.

Nipashe lilipomtafuta Lema kuthibitisha kauli hiyo, alikiri kuandika huku akisema amefanya hivyo kupisha demokrasia iamue na wajumbe waamue wanayemtaka katika kanda hiyo.

Alipoulizwa kuhusu kauli yake aliyoitoa wakati anarejea nchini kutoka Canada kwamba miongoni mwa vitu vilivyomsukuma kurejea ni pamoja na kuimarisha chama hicho na kutengeneza mikakati ya kupata ushindi katika kanda hiyo kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ujao, Lema alijibu kazi anaweza kufanya hata akiwa nje ya uongozi.

"Ni kweli, lakini kujenga chama naweza kufanya hata nikiwa nje ya nafasi na huo ni wito wa ki- Mungu ndani yangu isipokuwa kwa uongozi najisikia tu kuwa pembeni. Nimeacha demokrasia itawale na wajumbe wachague mtu wanayemtaka awaongoze," alisema Lema.

Kuhusu kugombea jimbo la Arusha Mjini, Lema alisema kwa sasa wanachoangalia ni uchaguzi wa serikali za mtaa.

"Sasa hivi tuko 2024, tuna wajibu mmoja kujenga mtandao wa chama kuelekea uchaguzi huo," alisema Lema.

Mmoja wa washirika wa CHADEMA, Wakili Boniface Mwabukusi, baada ya Lema kutoa kauli yake hiyo, aliibuka kwenye ukurasa wa kiongozi huyo na kuandika ujumbe chini yake akisema: "Kuna mahali tunakosea na tunajipa upofu kwa kivuli cha demokrasia, lazima tujitathmini.

"Tundu Lissu, John Heche, Peter Msigwa, Godbless Lema ni watu ambao chama chochote makini kinachoamini katika 'succession plan' hakiwezi kubeza kabisa umuhimu wao. Ngoja tuendelee kujilisha upepo."

Baada ya uchaguzi wa viongozi wa Kanda nne kwenye chama hicho, Kanda nyingine zilizobaki zinatarajia kufanya uchaguzi wake Julai, mwaka huu. Katika uchaguzi wa Kanda nne uliomalizika juzi, ni Kanda moja tu ya Victoria ambayo Mwenyekiti wa zamani, Ezekiah Wenje, ametetea nafasi yake huku zingine tatu za Serengeti, Magharibi na Nyasa zikiibuka sura mpya.

Katika Kanda ya Serengeti, aliyeshinda ni Lucas Ngoto kwa kumshinda aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Gimbi Massaba. Kanda ya Magharibi, aliyeshinda ni Dickson Matata akimbwaga aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Gaston Garubindi.

# Apandishwa kizimbani kwa mashtaka kuua mwanawe kisa kaiba 700/-

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKAZI wa Kijiji cha Chigunga, wilayani Geita, Stefano Mlenda (31), amepandishwa kizimbani Mahakama Kuu Kanda ya Geita kwa mashtaka ya kuua mtoto wake wa miaka tisa bila kukusudia.

Alipandishwa kizimbani jana mbele ya Jaji Mfawidhi Kevin Mhina na aliposomewa mashtaka, alikana kuhusika na kosa hilo na yuko mahabusu katika Gereza la Geita kwa kuwa kesi inayomkabili haina dhamana.

Baada ya mshtakiwa huyo kukana mashtaka dhidi yake, Jaji Mhina alimwambia Wakili wa Serikali, Scholastica Teffe amsomee maelezo ya awali.

Wakili Scholastica alidai mahakamani kuwa Novemba 16, 2023, saa moja usiku, katika Kijiji cha Chigunga, wilayani Geita, mtoto huyo inadaiwa aliiba Sh. 700 na kwenda dukani kununua soda.

Alidai kuwa mshtakiwa alimfuata mtoto wake huyo na kumkamata, akamfunga kamba miguuni na mikononi kisha kumcharaza fimbo maeneo mbalimbali ya mwili wake.

Wakili huyo alidai kuwa siku iliyofuata, mtoto huyo alifariki dunia na taarifa zilitolewa katika Kituo cha Polisi Butundwe, wilayani Geita na mshtakiwa alikamatwa na alipohojiwa kuhusiana na tukio hilo alikiri kuhusika na tukio la kumuua mwanawe bila kukusudia.

Alidai kuwa Novemba 18, 2023, daktari alichunguza mwili wa marehemu na kubaini mtoto huyo alifariki dunia kutokana na majeraha mbalimbali yaliyokuwa mwilini mwake.

Wakili huyo alidai upande wa Jamhuri unatarajia kupeleka mashahidi 11 na vielelezo vinne na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusilikiza mashahidi katika kesi hiyo.

Jaji Mhina alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Naibu Msajili atakapopanga tarehe ya kusikiliza kesi hiyo. Mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu katika Gereza la Geita.

# Waathirika mafuriko ya Rufiji wapatiwa mbegu za mahindi

**Na Mwandishi Wetu,** RUFIJI

WAATHIRIKA wa mafuriko yaliyotokea katika msimu wa masika mwaka huu wilayani Rufiji, mkoani Pwani wamekabidhiwa msaada wa mbegu za mahindi na Benki ya CRDB.

Msaada huo ni kilo 7,148.857 za mbegu za kisasa za mahindi zitakazosambazwa kwa wananchi ili wazitumie katika msimu ujao wa kilimo kuhakikisha wanakuwa na chakula cha uhakika. Zina thamani ya Sh. milioni 50.

Akikabidhi msaada huo uliopokewa na Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa benki hiyo, Tully Esther Mwambapa, alisema taarifa za athari zilizosababishwa na mafuriko yaliyotokea zimewasikitisha watu wengi ndio maana imekuwa rahisi kwao kutoa msaada huo utakaosaidia kurudisha shughuli za kilimo kwa uhakika.

"Majanga yana athari kubwa zinazorudisha nyuma uchumi wa watu na maendeleo ya taifa kwa ujumla. Mara zote, hutokea na kutukuta tukiwa hatujajipanga kukabiliana nayo au hatuna uwezo wa kuyazuia yasitokee.

"Hii ndio sababu iliyoishawishi benki yetu pamoja na kampuni zake tanzu kushirikiana bega kwa bega na serikali kukabiliana na majanga pindi tu yanapotokea ili kurejesha hali ya kawaida kwa waathirika," alisema.

Tully ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya CRDB Bank Foundation, alisema walipopata maombi ya uhitaji wa mbegu hizo kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohammed Mchengerwa, na Mbunge wa Rufiji, kwa ajili ya waathirika wa mafuriko, hawakufikiria mara mbili kwa kuwa waliona ni jambo litakalowasaidia waathirika kupunguza athari walizopitia na kurejesha hali zao kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele alishukuru benki hiyo, akisema kitendo ilichokifanya cha kukumbuka na kukimbilia waathirika wa mafuriko yaliyotokea ni cha kizalendo na kinachopaswa kuigwa na wengine.

"Moyo wangu na kichwa changu kama ilivyo kwa wana Rufiji wengi leo, vimejaa shukrani nyingi. Tunawashukuru sana kwa kutukimbilia kipindi hiki kigumu.

"Msaada huu wa mbegu za mahindi mnaotukabidhi leo umekuja kwa wakati mwafaka kwani utatusaidia kujikwamua kutoka katika athari za mafuriko kwa kupunguza gharama za kilimo, hivyo kutuhakikishia mavuno msimu ujao," alisema Meja Gowele.

Alisema mvua kubwa iliyonyesha mwaka huu imesababisha mafuriko yaliyoharibu mazao yaliyopandwa shambani na hata baadhi ya biashara, hivyo kurudisha wananchi wengi kwenye lindi la umasikini.






**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Anwani ya Simu: "Uvuvi"
Simu Nambari: +255(026)2322612
Nakushi: +255(026)2322613
Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz
Tovuti: www.mifugouvuvi.go.tz
Dodoma, 15 Mei 2024:

Mji wa Serikali-Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S. L. P 2847,
40478 DODOMA.

## TAARIFA KWA UMMA

### WARAKA WA MATUMIZI YA WAVU WA UVUVI (UVUNAJI) WA DAGAA KATIKA ZIWA VICTORIA KUANZIA TAREHE 15 JUNI 2024

*(Chini ya Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Uvuvi, Sura 279)*

1. Serikali, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), inalo jukumu la kisheria la kusimamia, kulinda, na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini. Vile vile, katika kusimamia na kuendeleza uvunaji endelevu wa zao la dagaa katika Ziwa Victoria, na maeneo mengine, Wizara inawajibu wa kusimamia Sheria na Kanuni zilizopo pamoja na kutoa nyaraka mbalimbali ili kukabili tishio la uendelevu wa rasilimali za uvuvi kutokana na mwenendo na mabadiliko katika tasnia ya uvuvi.

2. Kwa sasa imeonekana kuwepo kwa changamoto zinazotokana uvuvi wa dagaa wa kutumia wavu usiokuwa na ukomo (urefu na kina). Hali hii inasababisha wavuvi kuvua kwa wingi samaki wachanga aina ya sangara na aina nyingine ya samaki wasiokusudiwa, jambo ambalo linasababisha uharibifu wa mazingira, mazalia ya samaki na kutishia uendelevu wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria.

3. Hivyo, kwa mujibu wa majukumu niliyokasimishwa chini ya Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Uvuvi, Sura 279, natoa Waraka juu ya uvuvi wa dagaa katika Ziwa Victoria kama hatua ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi nchini kama ifuatavyo:-
   (a) Wavu wa dagaa utakuwa na urefu usiozidi mita sitini (60m) na kina cha mita ishirini (20m);
   (b) Umbali kati ya boya na boya usizidi sentimita tano (5cm);
   (c) Ukubwa wa tundu la wavu usipungue milimita nane (8mm);
   (d) Uvuvi huu ufanyike katika umbali usiopungua mita elfu mbili (2,000m) sawa na umbali usiozidi kilomita mbili (2km) kutoka ufukwe wa ziwa; na
   (e) Uvuvi huu hautafanyika mchana na wakati wa mbalamwezi kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 66(1) ya Kanuni za Uvuvi za 2009, kama ilivyorekebishwa kupitia Kanuni ya 16(d) (mm) na (nn) iliyotangazwa na GN 492 ya 03/07/2020.

4. Waraka huu umetolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi, hivyo basi, ukiukwaji wa aina yeyote ni kosa la kisheria. Aidha, Waraka utaanza kutumika rasmi 15 Juni 2024 kwenye maeneo yote ya Ziwa Victoria. Natoa wito kwamba sote tushirikiane kwani kwa ujumla hatua hii itasaidia katika kusimamia kikamilifu uvuvi wa dagaa. Pia, lengo mahsusi la Waraka huu ni kulinda ikolojia ili kuwa na uvuvi endelevu wa samaki, uhifadhi wa mazingira, na mazalia ya samaki katika Ziwa Victoria.

**Prof. Mohammed Sheikh**
**MKURUGENZI WA UVUVI**



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, akieleza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwenye mkutano wa hadhara wa ziara ya Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, mjini Manyoni jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mbunge ajichongea kwa Nchimbi kuomba uwaziri

**Na Romana Mallya,** SINGIDA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ameomba wananchi kutochagua viongozi wanaojali maslahi yao binafsi.

Ametolea mfano mmoja wa wabunge wa chama chake aliyemlalamikia kuwa amekuwa mbunge kwa mihula mitatu pasi na kuteuliwa hata kwa nafasi ya naibu waziri.

Balozi Nchimbi ametafsiri kauli hiyo ni ishara ya mbunge huyo kujali zaidi maslahi yake badala ya kuangalia wananchi anaowawakilisha bungeni.

Akizungumza jana katika kikao cha ndani na viongozi wa chama hicho mkoani Singida, wakiwamo madiwani, kilichofanyika mjini Singida, Balozi Nchimbi alisema kuchagua na kuchaguliwa ni haki ya mwanachama, hivyo wanapokwenda katika uchaguzi nia ni kuchagua wachache kuwawakilisha. "Haimaanishi tutachagua wenye uwezo sana au wenye akili, au wenye fedha na mali. Tunachotaka ni kupata wawakilishi, mtu ambaye akifika mahali ataongea kwa niaba yetu. Si fedha zake au mali.

"Nimewapenda wabunge wenu hapa wameongelea matatizo ya wananchi wao. Sehemu nyingine unakwenda ukikaa na mbunge anakwambia 'Mheshimiwa, unajua nimeshakaa bungeni miaka 15 hata unaibu waziri'.

"Unamwambia 'unaongea vitu gani wewe" Hayo ni mambo binafsi'. Wabunge wenu hakuna hata mmoja aliyeongelea cheo, wote wanaongelea matatizo ya wananchi na ndio uongozi tunaotaka," alisema.

Balozi Dk. Nchimbi alisisitiza wananchi wachague watu ambao watasimama mbele kwa niaba yao, akidokeza changamoto kubwa nyingine ambayo wanaipata sasa ni watu kutoruhusu waliochaguliwa kutimiza wajibu wao.

"Kwa sasa tupo katika hatua ya kuandaa wagombea. Mara nyingi tunaandaa wagombea, ukimuuliza sifa yake nini anakwambia 'ana hela huyu', huyu ana hela wa chama hiki cha wakulima na wafanyakazi," alisema.

Alisisitiza viongozi wakatae kutumika na kupima watu kwa uwezo wao na si kwa fedha zao.

"Ndio maana kuna wengine wanachaguliwa kwa fedha, akichaguliwa haonekani tena mpaka miaka mitano kwa kuwa anajua iliyopiga kura ni fedha si ninyi, kura kapigiwa na fedha zake. Atawaandalia fungu lingine miaka mitano atarudi na ninyi mnakwenda kuchagua kama ngedere," alisema.

Kuhusu nafasi ya mwanamke katika uongozi, Balozi Nchimbi alisema miaka minane iliyopita aliwaita watoto wake wa kiume na kuwaleza akipata taarifa au akiona wanapiga wake zao, moyoni wajue yeye kama baba anawadharau kupita kiasi.

"Mwanamke hapigwi, mwanamke hanyanyaswi, mwanamke anabembelezwa. Na ukipigania haki za wanawake kikamilifu utaona uwezo wao. Ndio maana leo tunaongelea kazi zilizofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Alipopata urais mara ya kwanza watu walikuwa na shaka, amethibitisha nafasi ameimudu, amethibitisha yeye ni mlezi wa Watanzania, anahangaika na wana CCM anahangaika na wapinzani, wote anawalea pamoja. Hakuna kiongozi aliyefanya mazungumzo mara nyingi kuliko yeye," alisema.

Aliagiza kila kiongozi atambue kuwa chama cha siasa si kampuni, bali chama cha watu, hivyo wafanye kazi kwa ushirikiano.

"Kama kuna watu wanapata tabu ni sekretarieti yangu kwa kuwa chama tumepewa kama watendaji wakuu, lazima tufanye kazi pamoja," alisema.

Balozi Dk. Nchimbi aliahidi kufuatilia kila hatua za ujenzi wa ofisi ya CCM Mkoa wa Singida ambao licha ya viongozi wake akiwamo baba yake mzazi kuanzisha jambo hilo mwaka 1984, hadi sasa ujenzi wake haujakamilika.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makala, aliwataka viongozi ndani ya chama hicho kutokuwa mabingwa wa kusikiliza, bali wajitahidi kutoa majawabu. "Wenzetu wale (vyama vya upinzani) wanasema 'Watanzania wamekuwa kama 'machawa', kila siku Samia Samia', wanataka tuseme nini?" alihoji.

Katibu wa NEC, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Rabia Abdallah Hamid, alisema utanzania ni jambo la kujisifia.

"Kwani wao wameweza wana nini na sisi tushindwe tuna nini? Nchi nyingi zimejaribu kuunda muungano, lakini wameshindwa, walioweza ni sisi Tanzania, walioshindwa ni nchi nyingine waliojaribu," alisema. Jana jioni, Katibu Mkuu Nchimbi alifanya mkutano wa hadhara katika siku ya pili ya kuhitimisha ziara yake mkoani Singida kisha kwenda Manyara na baadaye mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

## Madiwani wawaka gari la taka kubadilishwa matumizi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha limeelekeza Idara ya Mazingira ya halmashauri hiyo kuhakikisha gari la kubeba taka linafanya kazi yake ili Mji wa Mlandizi uwe safi muda wote.

Wamesema gari hilo litumike kulingana na malengo yaliyokusudiwa badala ya kufanya kazi nyingine na kuacha taka zikilundikwa mitaani na pembezoni mwa barabara.

Katika kikao cha baraza hilo kilichofanyika mjini Mlandizi jana, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Erasto Makala alisema idara hiyo inapaswa kufanyia kazi taarifa zilizotolewa na madiwani juu ya gari la taka kutofika kwenye baadhi ya maeneo kubeba taka. Hoja ya taka iliibuliwa katika kikao hicho na Diwani wa Kilangalanga, Mwajuma Denge aliyesema hali si nzuri kwenye maeneo ya barabarani na baadhi ya sehemu taka zinatupwa ovyo.

Diwani Denge aliomba kuwekwe mikakati madhubuti ya kuhakikisha gari la taka linafika maeneo yote na kuzoa taka zilizokusanywa ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Baraza hilo pia kwa pamoja lilikubaliana kushughulikiwa yeyote atakayehusika kutumia gari la kubebea taka kwa matumizi mengine.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kibaha Vijijini, Steven Shija alisema ni muhimu kuwa na utaratibu mzuri wa gari la taka kuzunguka mitaani kukusanya taka.

Katika kikao hicho, Kaimu Mkurugenzi Halmashauri hiyo, Fatuma Kisalazo alisema wamepokea maelekezo yaliyotolewa katika baraza hilo na watashughulika kuondoa vikwazo vilivyopo.

# 188,000 wachaguliwa kujiunga na kidato cha V, vyuo vya kati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANAFUNZI 188,787 waliokidhi vigezo, wakiwamo wenye mahitaji maalum 812, wamechaguliwa kwa kupangiwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano na vyuo vya kati kwenye fani mbalimbali kwa mwaka wa masomo 2024/25.

Muhula wa kwanza kwa wanafunzi wa kidato cha tano utaanza Julai Mosi mwaka huu, hivyo wote waliochaguliwa wanapaswa kuanza kuripoti shuleni Juni 30 na siku ya mwisho ni Julai 14 mwaka huu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, aliyasema hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari juu ya uchaguzi wa wanafunzi hao.

Mchengerwa alisema jumla ya watahiniwa walioandikishwa kufanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2023 walikuwa 572,359; wasichana 310,248 na wavulana 262,111. Alisema kati yao, watahiniwa wa shule waliosajiliwa walikuwa 543,332 (wasichana 293,122 na wavulana 250,210), watahiniwa wa kujitegemea walikuwa 29,027 (wasichana walikuwa 17,126 na wavulana 11,901).

"Ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja unaonesha watahiniwa 197,426 walipata ufaulu wa Daraja la I - III, hali inayoonesha ufaulu wa watahiniwa wa mwaka 2023 umeongezeka kwa asilimia 0.47 kulinganishwa na ufaulu wa Daraja la I - III wa watahiniwa 192,348 wa mwaka 2022," alisema. Mchengerwa alisema serikali imehakikisha wanafunzi wote wenye sifa wamepata nafasi kwenye shule na vyuo vya elimu ya ufundi.

Alisema kati ya wanafunzi hao walichaguliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka huu 131,986 (wasichana 66,432 na wavulana 65,554), wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari za kidato cha tano 622 zikiwamo mpya 82 zinazoanza mwaka huu.

"Wanafunzi hao wamepangiwa shule katika mchanganuo: Wanafunzi 1,462 (wasichana 669 na wavulana 793) wamepangwa katika shule za sekondari nane zinazopokea wanafunzi wenye ufaulu wa juu zaidi ambazo ni Kilakala, Mzumbe, Ilboru, Kisimiri, Msalato, Kibaha, Tabora Boys na Tabora Girls.

"Wanafunzi 6,576 (wasichana 3,449 na wavulana 3,127) wamepangwa katika shule za sekondari za kutwa za kidato cha tano. 123,948 (wasichana 62,636 na wavulana 61,312) wamepangiwa katika shule za sekondari za bweni za kitaifa za kidato cha tano," alisema.

Vilevile, alisema wanafunzi 56,801 (wasichana 17,332 na wavulana 39,469) wamepangiwa kujiunga kwenye kozi na fani mbalimbali za stashahada katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi vinavyosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sheria ziongezwe makali kuwadhibiti wabadhirifu

**TAARIFA** kuhusu ubadhirifu, uhamishaji wa fedha za serikali na matumizi kinyume cha malengo, yamekuwa masuala ya kawaida kusikika katika jamii ya Watanzania. Hali hiyo inatokana na taarifa zinazotolewa kwenye vyombo vya habari na taasisi zilizopewa mamlaka ya kufuatilia na kuchunguza matumizi ya fedha za serikali katika ngazi mbalimbali.

Miongoni mwa taasisi hizo ni Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA), kila mwaka, taarifa za taasisi hizo zimekuwa zikibainisha madudu katika matumizi ya fedha za umma yanayofanywa na baadhi ya watendaji katika serikali kuu na mamlaka za serrikali za mitaa.

Aidha, ziara za viongozi wakuu wa serikali, akiwamo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa zimekuwa pia zikieleza kwa kina namna fedha za umma zinazopelekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta kama elimu, afya, maji na barabara zinazoliwa au kuhamishwa na watumishi wachache wasio waaminifu katika halmashauri kwa kushirikiana na baadhi ya maofisa katika Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mwaka 2018, kwa mfano akiwaka katika ziara ya kikazi Mpwapwa mkoani Dodoma, Waziri Mkuu alibaini matumzi mabaya ya Sh. milioni 70 zinazotolewa kila mwezi kwa ajili ya kununulia dawa katika wilaya hiyo.  Kutokana na hali hiyo, Majaliwa alimwagiza aliyekuwa mkuu wa wilaya hiyo, Jabir Shekimweri, kuchunguza suala hilo ili kujua fedha hizo zinakwenda wapi.

Pia katika ziara yake mkoani mara mwaka huu, Waziri Mkuu aliibua ipigaji wa kutisha wa fedha za serikali katika halmashauri za Bunda, Butiana na Serengeti unaofanywa na baadhi ya maofisa wakiwamo wakuu wa vitengo vya fedha na uhasibu katika mamlaka hizo, ikiwamo kuhamisha fedha kupitia akaunti zao kwa kushirikiana na baadhi ya maofisa wa TAMISEMI.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, kwa mfano, ilibainika kuwa mkuu wa kitendo cha fedha na uhasibu alihamisha zaidi ya Sh. milioni 213.7 kwa uhamisho wa ndani kwa kushirikiana na ofisa wa TAMISEMI kwa kutumia akaunti zake binafsi za CRDB na NMB.


Aidha, katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, kwenye wilaya sita za mkoa huo, madudu makubwa yameibuliwa yakihusisha baadhi ya watumishi katika halmashauri wakitumia fedha kinyume cha utaratibu. Katika Halmashauri ya Arusha, maofisa 17 akiwamo mganga mkuu wa halmashauri, wamesimamishwa kazi kwa tuhuma  za wizi wa Sh. milioni 600.

Kama vile haitoshi,  katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli kuna watumishi wanadaiwa kuiba fedha za makusanyo kwa kutumia mashine za kielektroniki (POS) kisha kukimbilia kusikojulikana huku makandarasi wakiidai mamlaka hiyo mamilioni ya fedha kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule na uongozi wanawazungusha.  Hayo ni machache katika madudu mengi yanayofanywa katika taasisi mbalimbali za serikali zikiwamo mamlaka za serikali za mitaa. Kwa maneno mengine. Watu wamefanya taasisi hizo za umma sawa na shamba la bibi, yeyote aingiaye anajichumia kilichomo bila kuchukuliwa hatua.

Serikali kuu imekuwa ikipeleka mabilioni ya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo lengo kubwa na mahususi ni kuwaondolea wananchi adha mbalimbali wanazokutana nazo lakini wajanja wachache, waliopewa dhamana ya kuzisimamia na kutekeleza miradi hiyo kujichotea na kula wanavyotaka.

Kuendelea kwa vitendo hivyo,  kunaonyesha  dhahiri kwamba sheria zilizopo au kutokuchukuliwa hatua kali za kisheria watu wanaokutwa na makosa hayo, kunasababisha hali hiyo kuendelea. Ni wakati mwafaka sasa sheria kali zikatungwa ili kudhibiti vitendo hivyo au ikiwezekana, makosa hayo yaingizwe katika sheria ya rushwa na uhujumu Uchumi ambayo adhabu yake ni kubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hongera Wizara ya Afya kufanya uamuzi huu wa tumbaku, lakini...

**WIZARA** ya Afya imesema tayari bunge limepitisha Sheria ya Udhibiti wa Tumbaku ijulikanayo kama 'The Tobacco Products Regulation Act, 2003', inayotoa katazo la uvutaji sigara hadharani.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alibainisha hayo hivi karibuni jijini Dodoma wakati akijibu swali kutoka kwa mbunge aliyeuliza ni lini serikali italeta sheria ya kuzuia uvutaji wa sigara na mazao mengine hadharani.

Naibu Waziri huyo akasema, sheria hiyo imezuia matangazo ya tumbaku na bidhaa nyingine na tumbaku katika maeneo ya umma, ikiwamo vyombo vya habari, mbao za matangazo na kwenye matamasha.

Vilevile, Dk. Mollel anatoa wito kwa wabunge kuwa mabalozi wa udhibiti wa tumbaku katika jamii kwenye maeneo yao, ili kusaidia wananchi kuepuka magonjwa yasiyo yakuambukiza.

Pamoja na uamuzi huo wa wizara, ninadhani ipo haja ya kuchukua hatua zaidi kwa ajili ya kuokoa maisha ya Watanzania ambao si watumiaji wa tumbaku au bidhaa nyingine inayotokana na tumbaku.

Hatua ambazo zinafaa kuchukuliwa ni kutoa elimu ya kutosha kwa jamii kuhusu madhara ya tumbaku kupitia kwa wataalam wa afya ili waweze kujibu kitaalam hoja za wavutaji.

Imekuwa ni jambo la kawaida kukuta wavutaji wakivuta sigara katika mkusanyiko wa watu hasa kwenye vituo vya daladala au mtu amebeba mtoto huku akivuta dani ya usafiri wa binafsi huku akiwa na watoto.

Kwa hali hiyo, ni wazi wapo wengi ambao hawajui madhara ya kuvuta tumbaku, kwani wengine huwa wanahoji kwamba kama ina madhara kwa nini inalimwa au kwa nini kuna viwanda vya kutengeneza sigara?

Hivyo, ninadhani ipo haja kwa wizara yenye dhamana ya afya za Watanzania kujipanga zaidi, kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma wajue madhara ya uvutaji kisha waamue kuacha au kuendelea kuvuta.

Uelimishaji unaweza kuwa kwa njia ya mihadhara, kuunda klabu za kujadili madhara ya bidhaa za tumbaku shuleni, ndani ya jamii kwa njia ya vyombo vya habari na uandaaji na usambazaji wa vipeperushi na nyaraka mbalimbali za uelimishaji.

Mbali na hilo, uelimishaji unaweza kuwa wa kupitia mitandao ya kijamii, ushiriki na uelimishaji kwenye siku ya kuzuia matumizi ya tumbaku duniani, kama ambavyo itaadhimishwa siku chache zijazo.

Vilevile wadau wanaweza kushiriki na kutoa elimu katika maonyesho mbalimbali, elimu kupitia picha zinazoonyesha madhara ya kiafya, michoro na vibonzo lengo likiwa ni kuokoa Watanzania.

Wakati huu wa kuelekea katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Matumizi ya Tumbaku,ni vyema suala la elimu kuhusu madhara ya tumbaku likapewa mkazo ili kunusuru afya za Watanzania.

Mei 31 ya kila mwaka, huwa ni maadhimisho ya siku hiyo ambayo mwaka jana ilielezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Tedros Ghebreyesus kwamba tumbaku inasababisha vifo milioni nane kila mwaka duniani.

Aidha, anasema, zaidi ya ekari milioni 300 katika nchi zaidi ya 120 duniani zinatumika kwa ajili ya kilimo cha tumbaku hata kwenye nchi ambazo watu wake wana njaa kali.

Kwa kuwa lengo la maadhimisho ya Siku ya Kuzuia Matumizi ya Tumbaku Duniani, ni vyema jamii ikaelimisha hatari za matumizi ya tumbaku, ili kupunguza vifo vinavyotokana na matumizi ya tumbaku.

# Kilio malimbikizo ya walimu chasikika

**Na James Mwanamyoto,**
MULEBA

OFISI YA Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeanza kutekeleza maagizo yaliyotolewa kuhusu kutatua changamoto zinazowakabili walimu.

Katika kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Waziri wa Nchi TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Elimu), Dk. Charles Msonde, amewataka walimu wenye madai ya malimbikizo ya mishahara, kuwasilisha vielelezo kwa maofisa elimu ili wayashughulikie.

Dk. Msonde alitoa maagizo hayo kwa nyakati tofauti, wakati wa vikao kazi na maofisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu walioko katika halmashauri za wilaya za Biharamulo na Muleba mkoani Kagera.

"Walimu kuanzia sasa wasilisheni madai yenu na viambata vyake muhimu kwa maofisa elimu ili wao ndio wawasilishe kwa maofisa utumishi kwa ajili ya kushughulikiwa. Waziri mwenye dhamana, Mohamed Mchengerwa, alishaelekeza madai yote ya walimu yashughulikiwe," alisisitiza.

Dk. Msonde alisema maofisa elimu watekeleze jukumu hilo kwa kuwa wapo kwa ajili ya kuwahudumia walimu, hivyo ni wajibu wao kuwafuata Maofisa utumishi wakuu ili kushirikiana nao katika kushughulikia madai ya malimbikizo ya walimu.

Naibu Katibu Mkuu Msonde alihimiza kuwa ofisa elimu akishawasilisha madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi kwa ofisa utumishi mkuu, anapaswa pia kuwapatia mrejesho watumishi husika ili wajue ni hatua ipi imefikiwa katika kushughulikia madai yao.

"Ofisa elimu iwapo utaenda kwa ofisa utumishi na asikupe ushirikiano, nenda kwa mkurugenzi wa halmashauri na unijulishe mimi ili tuchukue hatua stahiki kwa ofisa utumishi ambaye anakaidi maelekezo halali ya waziri mwenye dhamana," alisisitiza.

Dt. Msonde alihitimisha siku ya kwanza ya ziara yake mkoani Kagera kwa kuhimiza uwajibikaji kwa maofisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu katika wilaya za Biharamulo na Muleba.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Kijamii (ESRF) Prof. Fortunata Makene (kulia), akizungumza katika wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga juzi, kuhusu utekelezaji mradi wa uvunaji maji ya mvua, watakaoutekeleza ndani ya miaka mitatu wilayani humo, ili kuwaondolea adha wanawake kufuata maji umbali mrefu hasa kipindi cha kiangazi ili kutopoteza muda wa kufanya shughuli za kiuchumi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Polisi wafukuzwa kazi sababu mashine kupimia mwendokasi

**Na Maulid Mmbaga**

ASKARI polisi wanane wamefukuzwa kazi na kufutwa jeshini na wengine kadhaa kesi zao ziko katika hatua ya mwisho baada ya kukutwa na hatia ya kutumia mashine za kupima mwendokasi (speed radar) kinyume cha maelekezo.

Taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi la Polisi, naibu Kamishna (DCP) David Misime, ilisema hatua hizo za kinidhamu ikiwemo kushtakiwa, zilichukuliwa baada ya uchunguzi uliofanyika hivi karibuni na kubaini kuwa askari polisi hao wa usalama barabarani walijihusisha na kitendo hicho.

Misime alisema kumekuwa na taarifa zinazosambaa mtandaoni zikitaka kuaminisha umma kwamba askari wa usalama barabarani wameingilia mfumo wa malipo ya fedha za serikali (POS) na kuchepusha fedha zilizotakiwa kuingia kwenye mfuko mkuu wa serikali.

"Kilichoko na kilicho sahihi ni kwamba Jeshi la Polisi mbali na kuwa na mpango kazi na mikakati ya kutekeleza majukumu yake, hufanya usimamizi na ukaguzi wa namna askari wanavyotekeleza majukumu yao ili kubaini ufanisi au ukiukwaji wowote ule.

"Hivyo mashine zilizotumiwa kinyume cha utaratibu kwa utashi na kwa manufaa binafsi ya hao askari ni za kupima mwendokasi na si zile zinazotumika kwa ajili ya malipo ya serikali (POS) kwani kuingilia mfumo huo si rahisi kama inavyoelezwa," alisema.

Aidha, alisema mashine aina ya POS zinazotumika kwa malipo ya faini za barabarani hadi sasa uchunguzi haujabaini kwamba mfumo umeingiliwa na fedha kuchepushwa kama ilivyodaiwa.

Hata hivyo, alisisitiza baadhi ya watu kuwa na subira na kusubiri ufuatiliaji unaofanywa na jeshi hilo kwa ajili ya kuwapatia taarifa sahihi pale wanapozihitaji kwa kuwa wasipofanya hivyo iko hatari ya kutoa taarifa zinazoweza kusababisha taharuki kwa umma.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Pinda aonya udanganyifu wa hatimiliki

**Na Munir Shemweta,** MLELE

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amewataka wananchi wanaokabidhiwa hati milki za ardhi kuhakikisha wanazitunza ili kuepuka udanganyifu unaoweza kufanyika kutoka watu wasio waaminifu.

Pinda alisema hayo juzi wakati wa hafla ya uzinduzi wa Wiki ya Mazingira iliyoambatana na ugawaji hati za hakimiliki za kimila za ardhi, Daftari la Usajili wa Wamiliki wa Ardhi la Kijiji na Vyeti vya Kijiji iliyofanyika kata ya Kasansa, Halmashauri ya Mpimbwe, Mlele mkoani Katavi.

Katika hafla hiyo ambayo mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Suleiman Jafo, hati za hakimiliki za ardhi za kimila 30 kati 4,450 zilizoandaliwa kupitia mradi wa urejeshwaji endelevu wa mazingira na uhifadhi wa bioanuai tanzania (SLR) unaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais zilitolewa.

Pinda ambaye ni Mbunge wa Kavuu, aliwatahadharisha wananchi kuwa hati milki za ardhi ni nyaraka na mali ambayo haipaswi kuazimishwa kwa mtu yeyote ili akachukulie mkopo benki bila kujua utaratibu wa namna ya kurejesha mkopo.

"Hii hati haiazimwi kama tunavyoazimana nguo. Ni mali na umsimgawie jirani hata mtoto wako ili aende akakopee bila kuwa na mpangilio maalum atarudishaje maana mwisho wa siku benki haitamwangalia aliyekopa bali kielelezo. Mtakuja kunyang'anywa mali kwa maana ya mashamba au nyumba, hivyo kazitunzeni,".alisema.

Pinda alisema iwapo mwananchi atashindwa kutunza hati milki ya ardhi, anaweza kuipeleka masijala za ofisi za serikali kama vile ofisi ya mkuu wa wilaya au mkurugenzi wa halmashauri ambao alisema wamepewa mweleko wa namna ya kutunza kumbukumbu ili wakati wa kutumia ukifika waende kuomba.

Aidha, Pinda aliiomba Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kupitia Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Uhifadhi wa Bioanuai Tanzania (SLR) kufadhili pia vijiji vingine vilivyoko kata za Mamba, Majimoto, Mbede, Usevya na Kibaoni katika halmashauri ya Mpimbwe ili kutunza mazingira sambamba na kuimarisha biashara ya hewa ya ukaa kwa lengo la kuleta manufaa kwenye vijiji vya kata hizo.

Waziri Jafo alipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa kufanikisha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na hatimaye kuandaa hati miliki za kimila 4,450.

"Hili ni jambo kubwa sana kufanikisha hati 4,450 na hapa peke yake ni hati 1,046. Ni faraja kubwa sana katika mradi huu, tumeona changamoto kubwa hasa watu wanaokosa hati za ardhi kupitia mradi huu tumeona mafanikio makubwa sana katika mustakabali wa maendeleo ya nchi," alisema.

Jafo alisema ofisi yake itatoa ushirikiano katika juhudi zozote za uhifadhi mazingira kwenye halmashauri ya Mpimbwe na mkoa mzima wa Katavi ili kuleta manufaa kwa mkoa na wananchi ikiwamo uvunaji hewa ya ukaa katika vijiji husika.

Kilele cha Wiki ya Mazingira kinachoambatana na shughuli mbalimbali nchini kama vile kongamano na shughuli za usafi, kitafanyika kitaifa Dodoma na kimataifa kitafanyika Riyadh, Saudia Arabia.

# TGNP yatoa neno dira mpya maendeleo

**Na Enock Charles**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP) umeshauri kuwekwa masuala ya jinsia katika dira mpya ya maendeleo ya taifa 2025-2050 ili mipango, mikakati na shughuli mbalimbali za maendeleo katika kila sekta na taasisi kuzingatia usawa wa jinsia.

Akizungumza katika mkutano wa vijana ulioandaliwa na mtandao huo, Ofisa Programu na Sera wa TGNP, Rogathe Loakaki, alisema licha ya mambo mazuri yaliyokuwamo katika dira iliyopita inayofikia tamati mwakani, masuala mengi yanayohusu haki za msingi kwa kuzingatia utofauti wa kijinsia hayakuwekwa.

"Masuala ya kijinsia yasipowekwa katika dira kila kiongozi atakayeingia madarakani atakuwa anakuja na vipaumbele vyake na pengine visiwe na mtazamo wa kijinsia, hivyo ni muhimu yakawekwa ili yatekelezwe kikamilifu," alisema Loakaki.

Mkurugenzi wa shirika la Bridge for Change, Ocheck Msuva, alisema ni muhimu kwa sauti za vijana kutokea katika dira mpya kwa sababu ndilo kundi kubwa kwa sasa na ambalo linatarajiwa kuishi muda mrefu na kuona utekelezaji wa dira hiyo.

"Kama una miaka 60 au 50 leo, pengine hutaishi uione lakini kijana wa miaka 25, 30 au 35 miaka 25 ijayo akiwa mzee sana labda atakuwa na miaka 60, hivyo ni rahisi kushuhudia utekelezwaji wa dira hiyo. "TGNP kama taasisi wangeweza kutoa tu maoni yao lakini kitendo cha kuwashirikisha vijana hawa ni kuheshimu mawazo yao ili yawemo katika dira mpya na hatutahariri mawazo yao yataenda kama yalivyo" alisema Msuva.

Mtandao huo ulialika vijana zaidi ya 50 kutoka katika vyuo na taasisi mbalimbali ili kutoa maoni yao yatakayopelekwa katika Tume ya Mipango na kujumuishwa katika mchakato wa maandalizi ya dira mpya 2025-2050.

Akizungumza katika mhadhara wa umma kuchochea mchakato wa kuandaa sera mpya za uchumi wa Tanzania kufikia mwaka 2050 jijini Dar es Salaam, Aprili, mwaka huu, Katibu Mtendaji ,Ofisi ya Rais-Tume ya Mipango, Lawrence Mafuru, alisema pamoja na mambo mengine ni muhimu dira hiyo ikalenga kuwakwamua wananchi katika umaskini. "Kuna maeneo ambayo tutayawekea kipaumbele katika dira mpya ya taifa ili kuhakikisha maendeleo tunayoyataka sasa yawe ni watu na si ya vitu kama ambavyo tumekuwa tukikumbushana.

Tunataka watu wetu wapate elimu itakayowawezesha kufanya shughuli za kitaalamu sio tu kumaliza chuo kikuu" alisema Mafuru. "Tutazingatia maeneo ambayo yanasababisha ukuaji wa uchumi kwa haraka maana yake ni kwamba kwa ukuaji wa uchumi kasi yake haijatusaidia kuondoa umaskini kwa kadri ambavyo tunataka," aliongeza.

Dira ya kwanza ya maendeleo iliishia mwaka 1999 ya pili ilianza mwaka 2000 na itaisha mwakani, hivyo kuwapo haja ya kuandaliwa dira nyingine ya mwaka 2025 hadi 2050.

# Mtendaji anusurika kifungo miaka mitatu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imemhukumu Mtendaji wa Kata ya Nyamwilolewa, Simon Maduka (34) kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. 500,000 baada ya kupatikana na hatia ya kupokea rushwa ya Sh. milioni moja kutoka kwa Pili Mwanzalima.

Hata hivyo, mshtakiwa amelipa faini ya Sh 500, 000 na baada ya kulipa, aliachiwa na kuondoka kwenda nyumbani kwake.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi Cleofas Waane baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Waane alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watendaji wa kata wengine wenye tabia kama yake.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Antidius Rutayuga, ambaye kuisuka kesi hiyo, alipeleka mashahidi tisa na vielelezo vitatu ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Waane alisema Aprili 4, 2023 mshtakiwa akiwa Mtendaji wa Kata ya Nyamwilolewa na akiwa katika kituo chake cha kazi, alipokea rushwa ya Sh. milioni moja kutoka kwa Pili Mwanzalima ili asimchukulie hatua za kisheria kwa kosa la kumhifadhi mhamiaji haramu, aliyejulikana kwa jina moja la Amos nyumbani kwake.

Katika kutoa hukumu hiyo, alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kubaini kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa pasipo kuacha shaka yoyote.

"Pia mahakama hii inakutia hatiani mshtakiwa kwa kosa uliloshtakiwa nalo na mahakama hii inakutaka utoe maombolezo ili kukupunguzia adhabu," alisema Hakimu Waane.

Mshtakiwa huyo alikuwa akitetewa na Wakili wa kujitegemea Daudi Mhagama ambaye alidai mahakamani kuwa mteja wake ni kosa lake la kwanza pia ana mama yake mgonjwa pamoja na familia inamtegemea, hivyo anaomba mahakama impunguze adhabu.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Kabura Benjamin, ulidai kuwa hauna kumbukumbu za makosa ya nyuma ya mshtakiwa lakini wanaomba mahakama itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Waane alitupilia mbali maombolezo ya mshtakiwa na kusema mahakama inamhukumu kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. 500,000 na akikosa kulipa atatumikia kifungo. Mshtakiwa pia alitakiwa kurudisha Sh. Milioni moja alizopokea rushwa kutoka kwa Mwanzalima.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Rutayuga alidai kuwa Aprili 4, 2023 katika ofisi ya mtendaji wa kata ya Nyamwilolewa mkoa wa Geita, mshtakiwa alipokea rushwa ya Sh milioni moja kutoka kwa Mwanzalima ili asimchukulie hatua kali za kisheria kwa kosa la kumhifadhi mhamiaji haramu.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTILINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KARIAKOO | MBM MOTORCYCLE SPARES | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 101, KITALU "47", HATI NAMBA 52425 | PETER SIMON MSANZYA | KIJITONYAMA -DAR ES SALAAM | 14/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | KOLE JOSEPH SAINI | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA P26009, HATI NAMBA DSMT1040275 | KOLE JOSEPH SAINI | BOMBAMBILI ILALA DAR ES SALAAM | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI | ZACHARIA ANTHONY KAPAMA | KIFURU KINYEREZI-ILALA | 12/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| HEAD OFFICE | FLORIAN CLAVERY RUGEMALIRA | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 300-SNGLR, KIWANJA NAMBA 794 &796 KITALU 'A' CHAPWA TUNDUMA | FLORIAN CLAVERY RUGEMALIRA | CHAPWA TUNDUMA | 17/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.SABA SABA MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 14/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| HEAD OFFICE | ALIPO BERNARD CHIKOKO | KIWANJA | ALIPO BERNARD CHIKOKO | BOKOTIMIZA-KIBAHA | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | CELESTINE MSIMBU SHIJA | KIWANJA | CELESTINE MSIMBU SHIJA | BOKOTIMIZA-KIBAHA | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | NELSON PETER SHOO | KIWANJA | NELSON PETER SHOO | BOKOTIMIZA-KIBAHA | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | MLOPA IDRISA SADALLAH | KIWANJA | MLOPA IDRISA SADALLAH | MAKURUNGE- BAGAMOYO | 19/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | ANNANEEMA DANIEL RITTE | KIWANJA | ANNANEEMA DANIEL RITTE | SEGU CHINI, KATA YA NALA - DODOMA | 17/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | ADAM DAVID KESSY | KIWANJA | ADAM DAVID KESSY | KISOPWA KWEMBE | 20/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MASOUD SALUM ALLY | NYUMBA | MWAJABU MOHAMED KONDO | TEMEKE | 17/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/0759282344/0784787981/0764461606**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.



## Wawili mbaroni kwa tuhuma za mauaji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoa wa Arusha linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za mauaji ya Ndembora Nanyaro, aliyefariki wakati akipatiwa matibabu baada ya kujeruhumiwa kwa kushambuliwa sehemu mbalimbali za mwili wake na watuhumiwa hao.

Akitoa taarifa hiyo jana jijini Arusha, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi (SACP), Justine Masejo, alisema watuhumiwa hao walimjeruhi Ndembora Mei 20 mwaka huu, katika Kijiji cha Ngurdoto, Kata ya Maji ya Chai Wilaya ya Arumeru.

Alisema baada ya kujeruhiwa Ndembora alipelekwa Hospitali ya KCMC na Mei 25 mwaka huu alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu.

"Jeshi la Polisi Mkoa Arusha linashikilia watuhumiwa hawa wawili, ambao majina yao yamehifadhiwa kwa sababu za kiupelelezi na pindi upelelezi utakapo kamilika watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria,"alisema.

Aidha, alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa chanzo cha shambulio hilo lililosababisha mauaji hayo ni ugomvi wa wana ndugu.

Alisema hata hivyo jeshi hilo linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo ili kubaini chanzo halisi cha mauaji hayo.

Masejo alitoa wito kwa wananchi kutojichukulia sheria mkononi, badala yake,wafike katika mamlaka zinazohusika ili kutatua matatizo yao. Alisema: "Lakini kuna viongozi wa dini embu pelekeni huko mkapate pia usuluhishi lakini siyo vizuri kujichukulia sheria mkononi na kusababisha vifo visivyo vya lazima".

## Amuomba Samia kumsaidia kupata haki ya nyumba

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MTANZANIA anayeishi nchini Uingereza, Anastazia Temu, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan (pichani) kuingilia kati mgogoro wa eneo la familia yao, akidai kuna baadhi ya watu wanataka kuwapoka.

Amesema kuna baadhi ya watu wanataka kuwapoka eneo hilo lililopo jijini Arusha ambalo wameishi kwa zaidi ya miaka 60

Akizungumza na Nipashe, Annastazia alisema eneo hilo lenye ukubwa wa takribani hekari mbili liko Kata ya Themi jijini Arusha, mkabala na bwalo la Polisi Arusha (Polisi Mesi).

Anastazia alisema kwa kipindi kirefu wametakiwa kuhama kwenye eneo hilo, akisema ni shinikizo kutoka kwa baadhi ya watu wenye ushawishi wa kifedha ambao wanalitaka.

Alisema kwa nyakati tofauti wamejaribu kwenda kwenye ofisi mbalimbali za serikali,l akini wameshindwa kusaidika kwa kuwa nguvu ya fedha imekuwa ikitumika.

"Tunatakiwa kutoka kwenye eneo la baba yetu na watu hao, lilikuwa ni la kwetu,baba alituachia kwa kuwa ndio yalikuwa makazi yetu ya kuishi mimi na ndugu zangu, tumezaliwa hapo, hivyo kwa niaba ya familia ninamwomba Rais Samia atusaidie ili tupate haki yetu kwa kuwa tumeteseka kwa muda mrefu na mtu pekee wa kutusaidia ni



wewe kiongozi wetu wa nchi," alisema.

"Baba yangu (Stansilous Temu), alipigana vita vya pili vya dunia na eneo lilikuwa lake, hata kabla ya nchi kupata uhuru mwaka 1961 na baada ya yeye kufariki aliliacha mikononi mwa familia na hivi tunavyozungumza tunatakiwa kuhama ili watu wachache walichukue kwa kigezo cha shirika," alisema.

Alisema mara nyingi anapokuja Tanzania inamlazimu kwenda kulala hotelini kwa kuwa kiwanja kilichokuwa na nyumba yao ya kuishi waliyokuwa wanaitegemea haruhusiwi kuliendeleza, hivyo hana sehemu nyingine ya kufikia.

Aidha, alisema ameufurahia mpango wa Rais Samia kwa kuigiza Filamu ya The Royal Tour ambayo ilikuwa na lengo la kutangaza kimataifa vivutio vya utalii vilipoko hapa nchini. "Na mimi hapa nilipo nimekuwa balozi mwema kutangaza utali kwa njia teknolojia na kuwa na duka ambalo vitu vyote vinavyopatikana Tanzania, hivyo ni kuunga mkono juhudi za kiongozi wangu ambaye ni mwanamke mwenzangu kwa kuwa amefanya kazi nzuri kwa maslahi ya kutangaza utalii wa nchi," alisema.

Nipashe lilifuatilia mgogoro huo na kubaini kulikuwa na kesi ya madai ya ardhi No.27/2020 ilifunguliwa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha na kusikilizwa na Jaji Joachim Tiganga.

Hukumu ya kesi hiyo, ilitolewa Agosti 28,2023 na iliwapa ushindi Shirika la YMCA kuwa ndio wamiliki halali wa eneo No.110A/1 na 110A/2 lililopo Kitalu E jijini Arusha kwa hatimiliki No.055025/20.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha **Nipashe** au **The Guardian** kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian





# MWAUWASA yafanya operesheni upatikanaji maji mitaani

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KAIMU Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Neli Msuya ameongoza watumishi wa mamlaka hiyo katika operesheni maalumu ya ufuatiliaji wa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mitaani. Operesheni hiyo ambayo imeanza kwa siku tatu ikifanyika katika maeneo yanayohudumiwa na Kanda ya Nyakato, kisha itahamia katika kanda nyingine lengo likiwa ni kubaini na kutatua kwa wakati maeneo yenye tatizo la upatikanaji wa maji.

Akizungumza wakati wa operesheni hiyo, Msuya alisema wanaendelea na jitihada za kuhakikisha huduma ya maji katika maeneo yote inaimarika kama ilivyo azma ya serikali kupitia Wizara ya Maji. "Tupo mitaani na watumishi wenzangu kufuatilia hali ya upatikanaji wa huduma ya maji, kukagua ufanisi wa mfumo wa usambazaji maji kwa maana ya bomba na dira za maji, kuzungumza na wateja na kusikiliza maoni yao, kufanya maboresho madogo ya kimfumo sambamba na kufuatilia madeni ya muda mrefu," alisema Msuya. Aidha, aliwakumbusha wateja kuhakikisha wanalipa ankara zao kwa wakati ili kuiwezesha MWAUWASA kuendelea kuboresha huduma na kuwa wanatoa pia elimu ya matumizi sahihi ya maji, usomaji shirikishi wa dira, namna ya kutoa taarifa.

Baadhi ya wananchi waliofikiwa na huduma hiyo akiwemo, Hussein Obama alisema hatua hiyo imekuwa msaada hasa katika marekebisho ya miundombinu ambayo imekuwa ikiharibiwa na ukarabati wa miundombinu ya barabara.

# NSSF yaagizwa kushughulikia matatizo ya wastaafu

**Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda ameutaka Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kujikita zaidi katika kushughulika na utatuzi wa matatizo yanayowakabili wastaafu nchini.

Mtanda alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wastaafu watarajiwa ambao ni wanachama wa mfuko huo wakati akifungua semina ya mifumo ya tehama kwa wastaafu watarajiwa 400 iliyofanyika jijini Mwanza.

Mtanda alisema kwa uzoefu aliokuwanao kupitia uenyekiti wake wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii amebaini kuwa hifadhi za jamii haziwezi kujitenga na maslahi ya wazee kwa kuhakikisha wanajengewa msingi wa kutoa pensheni kwa kundi hilo.

Aidha, aliwataka wastaafu hao watarajiwa kujiandaa na kuwa na maamuzi kwa kuwa na vitega uchumi kabla ya kustaafu na kupanga wapi wanakusudia kwenda kuishi, kwani maisha ya mjini yanatofautiana na ya kijijini kutokana na kuwa na asili tofauti ya mahitaji na aina ya shughuli za kuwekeza.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu NSSF, Robert Kadege, alisema mfuko huo unatoa mafunzo hayo kwa wastaafu watarajiwa juu ya kustaafu bila hofu, mafao na ukokotozi wa mafao pamoja na masuala ya afya.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda (kulia), akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja Mauzo wa kampuni ya Urus Tanzania, Meshack Anacleth kuhusu namna kampuni hiyo inavyowezesha upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora za ng'ombe wa maziwa na nyama, alipotembelea Maonyesho ya 27 ya Wiki ya Maziwa yanayoendelea, jijini Mwanza jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Kamati ya amani yaomba 'sapoti' kukemea uhalifu

**Na Vitus Audax,** MARA

KAMATI ya amani na maridhiano mkoani Mara imeiomba serikali mkoani hapa kuiunga mkono katika utekelezaji wa majukumu ya kiofisi ikiwa ni pamoja na kuwezeshwa katika safari za kila wilaya ili kukemea vitendo vya uhalifu na uvunjifu wa amani.

Katibu wa Kamati hiyo, Shekhe Juma Masiloli alitoa ombi hilo juzi katika kikao cha pamoja baina ya kamati hiyo na Mkuu wa Mkoa wa Mara.

Shekh Masiloli alisema baadhi ya viongozi wa taasisi za serikali hawatoi ushirikiano kwa kamati hiyo jambo ambalo linawakwamisha katika utekelezaji wa majukumu yao, hivyo kumuomba ofisi ya mkuu huyo wa mkoa kusimamia swala hilo.

Aidha, aliwasilisha maombi ya kamati hiyo ya kupatiwa Sh. milioni moja kwa ajili ya kulipia ya pango la ofisi pamoja na mafuta lita 140 kwa ajili ya ziara watakayoifanya katika wilaya tatu za mkoa huo.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi aliwaomba viongozi hao wa dini kuendelea kuisaidia serikali katika kukemea maovu mbalimbali katika jamii ikiwemo vitendo vya wananchi kujichukulia sheria mkononi katika mambo yanayotakiwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

"Tukemee mauaji ya mara kwa mara, ukatili, mapigano ya kutumia silaha katika migogoro pamoja na masuala ya ulawiti na ubakaji wa watoto wadogo shuleni na katika jamii" alisema Mtambi.

Aidha, alisema katika kukabiliana na changamoto wanazokabiliana nazo kama kamati watahakikisha kila mwezi wanakuwa na kikao cha pamoja ili kumfikishia kujadili masuala mbalimbali na namna ya kufanikisha vita dhidi ya vitendo hivyo.

# Wanafunzi 10,000 Biharamulo hawajulikani walipo

**Na Vitus Audax,** BIHARAMULO

WANAFUNZI zaidi ya 10,000 waliosajiliwa kujiunga na elimu ya msingi na sekondari katika shule zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo hawajaripoti. Taarifa hiyo ilitolewa na baadhi ya madiwani wakati wa kikao cha baraza kilicholenga kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Walisema sababu kubwa ya anguko la wanafunzi wilayani humo ni pamoja na kutembea umbali mrefu na uhaba wa walimu. Walisema ili kunusuru hali hiyo serikali inatakiwa kufanya mgawanyo sawa wa walimu katika maeneo ya mijini na vijijini ili shule za pembezoni ziwe na mwendelezo mzuri wa ufundishaji. Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatuma Mwasa aliwaagiza watendaji pamoja na viongozi wa idara za elimu kuwasaka wanafunzi hao zaidi ya 10,000 na kuhakikisha wanapelekwa shule na kuendelea na masomo.

"Hawa ni wanafunzi wengi sana wako wapi?, nina wasiwasi hata wanaposema wamesajili hawa watu wanakuwa hawakusajiliwa idadi hiyo nendeni mkaanze na darasa la kwanza pamoja na kidato cha kwanza katafuteni madarasa yote waliotajwa kuwa wamesajiliwa kama ndio wapo,"alisema Mwasa. Alisema halmashauri hiyo haina biashara yoyote kubwa ambayo ingetajwa kuwa sababu ya wanafunzi hao kukimbilia huko na kuacha kwenda shule.



Ukurasa 12

**Wachina wawapa ofa kinamama mashine za mil 79/- kutotoa vifaranga, wakimpigia makofi Samia**




Ukurasa 13

Kiswahili tunakifukuza wenyewe nchini


# BUFE

IJUMAA MEI 31, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 14

**RC awafuata wakulima shambani kuweka sawa dai lao 'zao pamba halilipi'**

WAKIENDELEZA MBEGU ZA WAKONGWE...

# Dk. Samia anakanyaga Korea Kusini, akitarajiwa kurejea na mazito matatu

**Na Peter Orwa**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, anaanza ziara ya siku sita nchini Korea. Ni tukio linalotazamwa ndani yake kinabeba sura pana ya uhusiano kisasa, kihistoria, undugu, pia diplomasia uchumi ambayo ndio sera na muongozo mkuu wa Tanzania nje ya mipaka.

Suala la uwekezaji katika sekta ya kilimo kuwa mlishaji taifa na hata nguzo ya kuajiri, Korea Kusini ina undugu wa kitaifa, tangu mikakati ya awali ya uchumi wa nchi, katika Serikali ya Awamu ya Kwanza.

Ziara ya sasa ya Dk. Samia, anatarajiwa kurejea nchini na mambo makuu matatu; mikataba saba ya maendeleo, pia mkataba wa mkopo nafuu Dola za Marekani Bn. 2.5 sawa na Sh.Trilioni 6.5 za kuwekeza katika miundombinu, elimu na afya kama alivyodokeza, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano Kimataifa,

Pia, anatarajiwa kurejea na shahada ya uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Anga Korea (KAU). Hadi sasa ana zingine kama hizo alizopewa na vyuo vikuu vya Dar es Salaam (UDSM), Zanzibar (SUZA) nchini, pia Jawaharal Nehru (India), Ankara (Uturuki).

Ni jambo lionalomuanika Rais Dk. Samia, mbali na uzoefu kikazi, kitaaluma, kichwani alivyowekeza darasa la elimu ya takwimu katika ngazi ya diploma nchini, pia stashahada ya uzamili katika uchumi, huko Manchester Uingereza, leo anayotenda yanayomuonyesha stadi yake katika fani uchumi, ameiva.

Hiyo ni mara baada ya kukakalia nafasi ya urais, Dk. Samia hakuficha dhana yake kusimamia mambo makuu matatu katika mikakati ya uchumi wa Tanzania nje ya mipaka.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipozungumza na Balozi wa Korea Kusini Nchini, Kim Sun Pyo (kushoto) Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu, Magogoni, Dar es Salaam, mnamo Oktoba 2022. **PICHA: MAKTABA**

Rais ambaye wiki hii anazawadiwa stashahada ya udaktari wa falsafa ya tano, kutoka Chuo Kikuu cha Anga (KAU) nchini Korea Kusini, anapigania kuimarisha Tanzania ing'are katika diplomasia uchumi, ziara zake zimekuwa zikilenga kunasa masoko ya bidhaa za nyumbani ughaibuni.

Vyuo vikuu vilivyompa tuzo kama hiyo ya uzamivu vya Dar es Salaam (UDSM), Zanzibar (SUZA) nchini, pia Jawaharal Nehru (India), Ankara (Uturuki).

Maeneo mengine alikojipanga kukuza uchumi kimkakati nchini, ni pakukaribisha uwekezaji mitaji hasa ya viwanda na kwenye kilimo na ushirikiano wa jumuiya/urafiki kimataifa, wakati huohuo, ikinakshi nchi kwa urafiki kisiasa.

Neema zinashuhudiwa, pale misaada ya kifedha, uwekezaji na jina la nchi kimataifa kilipaa, mahsusi hata mwenyewe Rais, imekuwa kama sheria ndogo, kila anakoalikwa au kufanya ziara ni kawaida anakaribishwa kuwasilisha ama mada, hotuba au kuongoza kikao. Si haba, Tanzania inang'ara kupitia Mama 'anayeupiga mwingi.'

**TANZANIA ILIKOTOKA NAO**

Tangu zama za uongozi wa Awamu ya Kwanza uongozi wa Tanzania na Korea Kusini, zimekuwa na historia kusaidiana kuwapo miradi hasa ya kilimo, ikijumuisha kusomeshwa Watanzania elimu ngazi hadi ya shahada za juu.

Pia, nchi hiyo imekuwa na baadhi ya miradi ya kilimo katika mikoa kama ya Morogoro, tena ikitumia wataalamu wengi wasomi Watanzania wahitimu wa nchi hiyo.

Ni aina ya uhusiano endelevu kufika zama za sasa, katika Awamu ya Nne ya uongozi wa nchi, taifa hilo la ukanda wa Mashariki ya Dunia, ikitia saini yamiradi ya kilimo nchini.

**SAMIA VS KOREA KUSINI**

Mkakati wa Rais Dk. Samia, katika falsafa yake ya kujenga Tanzania yenye kilimo cha kisasa na biashara, Julai mwaka jana zimeingia katika makubaliano ya kushirikiana kufanyika utafiti wa kilimo chenye teknolojia ya kisasa, ambayo katika miaka miwili ya mfululizo bungeni, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe amekuwa akiinadi.

Nchi za Tanzania na Korea Kusini, hadi sasa zimeshakubaliana kushirikiana katika kuimarisha utafiti wa kilimo na matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kilimo, ili kuongeza tija kwa wakulima nchini, mwaaka huu.

Hapo kukafafanuliwa lengo la kuwapo tija kwa wakulima shambani, jijini Jeonju-si, Korea Kusini, katika mazungumzo ya Naibu Waziri wa Kilimo wa Tanzania Anthony Mavunde na Yun Jongchul, Makamu Mtawala Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Kilimo na Utafiti ya Korea (Korea Patnership for Innovation in Agriculture - KOPIA).

Kupitia mazungumzo hayo, Naibu Waziri Mavunde akaiomba KOPIA kuanzisha kituo chake nchini Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), ili kubadilishana uzoefu na kuongeza ufanisi katika utafiti kilimo, lengo ni kumsaidia mkulima kufikia tija ya uzalishaji shambani.

Hapo kunazugumziwa maeneo ya mbegu bora na teknolo-


INAENDELEA UK.14

UCHUMI

# Wachina wawapa ofa kinamama mashine za Mil. 79/- kutotoa vifaranga, wakimpigia makofi Samia

**Na Sabato Kasika**

HADI sasa katika azma na dhamira ya serikali imedhamiria kuwezesha na kuinua wanawake kiuchumi, kutokana na juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kuwapa mitaji ya fedha na kuwatafutia vitendea kazi kwa wafadhili.

Ipo mifano mingi, miongoni mwake ni msaada wa hivi karibuni wa cherehani 425 na mashine 250 za kutotolea vifaranga vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 79 vilivyotolewa na serikali ya China.

Msaada huo ulikabidhiwa kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima na Balozi wa China hapa nchini, Chen Mingjian.

"Cherehanii hizi na mashine ya kutotolea vifaranga, tutashirikiana na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake ya CCM Taifa (UWT), mama yetu Mary Chatanda kuwatafuta wanawake tutakaowaibua hasa wenye uhitaji na kuwapelekea," anasema Dk. Dorothy.

Anafafanua kuwa wajasiriamali 675 watanufaika na msaada huo, huku cherehani 300 na mashine zote za kutotolea vifaranga vitapelekwa katika vikundi vinaratibiwa na wizara yake, lakini cherehani 125 vitapelekwa kwa vikundi vilivyo chini ya Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT).



Balozi wa China nchini, Chen Mingjian kulia na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, wakimkabidhi Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda, moja ya cherehani hizo. **PICHA: SABATO KASIKA**

Dk. Dorothy anasema vyerehani na mashine hizo, zinagusa ahadi mbalimbali za Rais Samia Suluhu Hassan za kuwezesha wanawake kiuchumi, na kwamba yeye (Rais) ni kinara wa kuwezesha wanawake.

"Wanajitokeza marafiki wa Tanzania walioilewa falsafa ya Rais Samia. Sisi wizarani tunapokea wageni wengi wanauliza kuna nini kwa wanawake, tunawapa takwimu na kuwaeleza programu ya kuwezesha wanawake kiuchumi ambayo kinara wake ni Rais Samia," anasema.

Anasema hadi sasa serikali inatekeleza Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 inayotoa kipaumbele kuwezesha wanawake kiuchumi pamoja na kuondoa ukatili wa kijinsia.

"Serikali inatambua umuhimu wa wanawake kushiriki katika shughuli za kiuchumi, hivyo msaada huu wa ndugu zetu wa China, utakuwa chachu kwenye programu ya uwezeshaji wanawake kiuchumi," anasema.

Aidha, anasema hadi sasa, kupitia mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi, tayari Sh.bilioni 743.7 zimeshatolewa na kunufaisha Watanzania 6,064,957, wakiwemo wanawake 3,556,359 sawa na asilimia 54, wanaume wakiwa ni 3,288,186 sawa na asilimia 46.

**NENO TOKA UWT**

Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda anasema kampeni za uchaguzi zinahitaji fedha na kuongeza kuwa wanawake wengi hawana vipato vya kutosha, na kwamba hatua zinazochukuliwa na serikali za kuwezesha wanawake kiuchumi zitawafanya wajitokeze kwa wingi.

"Umaskini wa kipato unawafanya wanawake wengi kubaki nyuma, lakini ninaamini wakiwezeshwa kiuchumi, wanaweza kupambana na wanaume hadi tukafikia asilimia 50 kwa 50 tunayoitafuta," amesema Mary.

Anasema UWT imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kutaka kuwainua wanawake kiuchumi ikiwamo msaada wa vifaa vya uzaalishaji mali na pia kutoa elimu ya kuwawezesha kupata mikopo.

"Tunawahamasisha kujiunga katika vikundi, ili wapate mikopo ikiwamo inayotolewa na halmashauri, lakini kuna msaada wa vitu ambalimbali tunaopata ukiwamo huu vyerehani kutoka China," anasema.

Mary anasema, kwa sasa umoja huo unajiandaa kuzunguka nchi nzima kwenda kushirikiana na maofisa maendeleo ya jamii kwa lengo la kutoa elimu kwa wanawake jinsi ya kutumia mikopo.

"Kuna mikopo inayotolewa na halmashauri zetu, tunataka tuwafundishe jinsi ya kuipata na kuitumia kwa usahihi, sio kwenda kununua vitenge, kwa sababu ehaviwezi kurejesha mkopo," anasema.

Anasema, wanawake wakiimarika kiuchumi, wana uwezo wa kuwania uongozi na kushinda bila kuingia katika mtego wa rushwa ya ngono ambayo wamekuwa wakikumbana nao na kuamua kukaa pembeni.

"Bila nguvu kiuchumi, ushiriki wa wanawake katika siasa unaweza kuwa kitendawili na kuongeza kuwa ni muhimu kutekeleza Azimio la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), linalotaka ushiriki wa wanawake na wanaume katika fursa za uongozi kuwa 50 kwa 50 ifikapo mwaka 2030," anasema.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian anasema, nchi yake imekuwa ukitoa misaada mbalimbali ya kuwanufaisha wanawake wa Tanzania, ili kuimarisha ustawi wa wananchi, na kwamba waliotoa utawasaidia walengwa kuongeza kipato.

"Kwa miaka miwili ambao nimefanya kazi Tanzania, nimejionea Rais Samia akitilia mkazo masuala yanayohusu wanawake na kushuhudia baadhi ya wanawake wenye uwezo mkubwa," anasema Chen.

Anasema, China na Tanzania zina ushirikiano mzuri, na kufafanua kuwa anafurahi kuona ushirikiano huo unazaa matunda, na kwamba China ilishwahi kutoa mbegu za soya kwa wakulima wa mkoa wa Ruvuma.

Vilevile, tumeshirikiana na taasisi isiyo ya serikali kutoa taulo za kike kwa ajili wa kusaidia wasichana na wanawake, hili limekuwa na mafanikio na tangu nimekuja Tanzania," anasema.

Balozi huyo anasema, wanawake wa Tanzania wanajitihidi kuendelea kukuza uchumi wao, na kwamba serikali ya China na Tanzania nazo zinasaidia kuwawezesha kiuchumi ili kuwapa unafuu wa maisha.

# Taasisi yaungana na Bashe kumsogezea PPP mkulima kutekekeleza anachokinadi

**Na Mwandishi Wetu**

HADI sasa nchini, kuna mageuzi makubwa ya kisera, kutoka kilimo cha mazoe hadi kwenye kisasa.

Hiyo inaendana mageuzi maradufu katika bajeti inayoelekezwa katika sekta hiyo, haja ni kukidhi lengo la mageuzi hayo.

Mtazamo huo, ambao umehubiriwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassana mara kadhaa, huku katika mawasilisho ya waziri mwenye dhamana, Hussein Bashe, ni yakina kwamba kilimo kiwe mwajiri na kiendeshwe kibiashara, kwa zana na teknolojia bora, ikiizingatia dhana ya umwagiliaji.

Sasa kuna miradi ya mfani kutekeleza hiyo ikiwamo unaoitwa BBT, ukijenga tafsiri ya kumjengea maisha kijana.

Aidha, kilimo hicho kinachoendeshwa katika mfumo shirikishi, kati ya sekta binafsi na umma ambayo ina sheria yake (PPP), huku mapinduzi ya viwanda yakiendelezwa kwa sera na mikakati, kutumia malighafi ya mapinduzi kilimo.

Mustakabali unaokaziwa zaidi ni nchi kujitegemea kwa mahitaji ya shambani, chakula na malighafi yanayopatikana nchini, pia sekta hiyo ijali maradufu, kama ilivyo malengo tangu uhuru wa nchi mwaka 1961.

Hapo ndipo mdau wa PPP, Kampuni ya Serengeti Breweries, sasa imejitokeza katika dhamira hiyo kushirikiana na serikali katika kuwanufaisha wakulima nchini kwenye mnyororo mzima wa thamani wa mazao yao.

Kampuni hiyo inasema kwamba imefurahishwa na azma ya serikali kupitia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2024/25 iliyojikita katika kuimarisha uzalishaji wa kilimo, kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, kupanua upatikanaji wa masoko kwa bidhaa za kilimo, na kuwawezesha wakulima wadogo nchini.

Kampuni hiyo inafafanua ni hatua inayofungua njia kwa mashirika na kampuni binafsi kunufaika na msaada unaotolewa na serikali katika kuboresha mazingira ya kilimo nchini.

"Kwa kuongeza mahitaji ya mazao yao, ushirikiano huu baina ya SBL na wakulima unahakikisha kuinua kipato cha wakulima na hivyo kuboresha maisha ya kaya vijijini, pamoja na kutanua wigo wa kodi kwa serikali." anasema Neema Temba, Meneja Uhusiano wa kampuni hiyo.

Hadi sasa taasisi hiyo binafsi, mbali na uzalishaji wake wa asili, ina miradi ya kilimo biashara ya kuwasaidia wakulima wanaozalisha mazao ya mahindi, mtama mweupe na shayiri katika mikoa mbalimbali nchini.

Kupitia mchakato huo, imeongeza mahitaji ya matumizi yake ya malighafi zinazopatikana ndani ya nchi kutoka asilimia 60 mwaka 2020 hadi asilimia 80 kwa mwaka jana, Neema anasema kuwa zaidi ya tani za ujazo 20,000 za malighafi zinatumika kwa mwaka katika mchakato wa utengenezaji bia wa kampuni hiyo.

Programu hiyo ya kuwasaidia wakulima wazawa imejikita katika maeneo makuu tisa tofauti ambayo ni pamoja na kufanya vipimo vya udongo, kemikali, upatikanaji wa mikopo, mbegu bora, matumizi ya mashine, bima ya mazao, mbolea, mafunzo, na mikataba ya ununuzi inayoweza kuingiwa upya kila mwaka kulingana na utendaji wa wakulima.

Mazao haya ya shayiri, mahindi na mtama mweupe yananunuliwa kutoka mikoa mbalimbali nchini ikiwamo Iringa, Morogoro, Mbeya, Singida, Dodoma, Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Kupitia mkakati huo wa kilimo cha mkataba baina ya SBL na wakulima, kampuni hiyo inalenga kununua zaidi ya tani 8,500 za shayiri na zaidi ya tani 6,500 za mtama mweupe katika mwaka wa fedha 2024.

"Mkakati wetu wa ugavi wa ndani unachangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza maoni ya serikali ya kuwainua wakulima wa ndani, hivyo kuipa nguvu sarafu ya nchi kwa kupunguza utegemezi mkubwa wa kuagiza malighafi kutoka nje ya nchi. Kwa kutoa kipaumbele katika ugavi wa ndani," anaongoza Mkurugenzi wa Mahusiano John Wanyancha.



Mkulima wa shayiri akiwa shambani, moja ya mazao yanayofanyiwa kazi na taasisi binafsi kuiunga mkono serikali. **PICHA:MTANDAO**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Kiswahili tunakifukuza wenyewe nchini






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

ALHAMISI, Mei 23 mwaka huu nikifuatilia matangazo ya Bunge kutoka Dodoma, nilimsikia Mbunge wa Kilosa, Profesa Palamagamba Kabudi, akichangia hotuba ya Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, kwa hisia kali.

Profesa Kabudi katika mchango wake, alionekana kujikita zaidi katika lugha ya Kiswahili, akieleza jinsi inavyobanangwa na Watanzania wenyewe wanaoaminika kuwa ndio wenye asili ya lugha hiyo adhimu duniani.

Msomi huyo mbobevu, mwanazuoni wa siku nyingi wa Sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alitaka hatua zichukuliwe ili kuokoa lugha hiyo, hasa kutokana na ukweli kuwa dunia karibu yote inaamini bila Tanzania, hakuna Kiswahili.

Alifikia hatua akagusia kuwa moja ya nchi jirani zinazotumia Kiswahili ambazo awali zilitegemea sana Tanzania kwa mafunzo ya lugha hiyo kwa watu wake, kufikia hatua ya sasa kutaka wasije nchini kujifunza lugha hiyo, kwani inaonekana hata sisi tunaanza kuipa kisogo na kukiharibu.

Alitoa mfano wa baadhi ya maneno yanayobanangwa, kama vile badala ya kutamka 'haya' inatamkwa 'aya', 'huyu' inakuwa 'uyu', 'habari' inakuwa 'abari' na kadhalika. Haina ubishi, kwamba hata lafudhi za baadhi ya makabila nchini zinaathiri Kiswahili.

Wapo Watanzania wasio na 'l' bali 'r' hivyo si nadra kumsikia akitamka 'chakura' badala ya 'chakula' au 'mari' badala ya 'mali', hali kadhalika wasio na 'r' bali 'l' katika maneno kama 'balabala' badala ya 'barabara', 'mahali' badala ya 'mahari'.

Yapo makabila yasio na 'ng', ambao 'ng'ombe' wanaita 'ngombe' na 'ng'ang'ana' watatamka 'ngangana' na wengine 'nchi' wakitamka 'nji' na matamshi mengine mengi kama hayo, yanayosababisha Kiswahili kiende harijojo katika matumizi yake.

Lakini, Profesa Kabudi hakuishia hapo, alifikia kusema kuna baadhi ya maneno yameachwa kutumika kwa wasiwasi tu wa watumiaji wa lugha hiyo wakidhani pengine kuyatamka si sawa, kama vile matiti kuitwa maziwa au nyonyo.

Alisema hapana sababu ya watu kushindwa kutamnka matiti, maneno ambayo yametumika miaka nenda rudi bila matatizo, ila tu watu kwa maslahi yao au kwa shaka walizonazo, wanabadilisha na kupoteza maana.

Alikubaliana na maneno ya tafsida ambayo hayawezi kutamkwa, zikiwamo sehemu za siri na matumizi yao, ambavyo haviwezi kutamkwa moja kwa moja na badala yake kutumia tafsida.

Namuunga mkono Profesa kwa kuliona hilo na kulisemea, ili wizara husika ichukue hatua ya kukuza Kiswahili, ili majirani wasitukimbie na hata kutupora dhima ya kukifundisha kwa jamii zetu na zingine kimataifa.

Mathalan, kuna sababu gani ya kusindwa kutumia misamiati katika usahihi wake, tukishindwa kutumia mashikio au makamatio badala ya mikono, matembeleo badala ya miguu, maoneo au matazamio badala ya macho?

Ni kweli, kwamba lugha ya Kiswahili imeendelea kuharibiwa siku hata siku kutokana na matumizi mabaya, huku wizara husika ikiendelea kutazama na kulea wanaoibananga bila hatua yoyote.

Tunashuhudia wasomi wengi wakidhani kuwa kusoma ni kuachana na Kiswahili na ndio wamekuwa wakiongoza kukiharibu kwa kuzungumza wakichanganya na Kiingereza, pia wasanii wa kizazi kipya ambao wanadhani bila kuimba Kiingereza hawajafanikiwa. Ni ulevi tu!

Kwenye vyombo karibu vyote vya habari vya kielektroniki, kwa maana ya televisheni na redio, tukifuatilia vipindi vingi vya michezo na baadhi visivyo vya michezo, vina majina ya Kiingereza. Sababu ni nini? Ni ulimbukeni tu.

Tukisikiliza vipindi vinavyochambua michezo, huko ndiko Kiswanglishi kiimekaa. Wachambuzi wanajisahau wakichambua kana kwamba ni kwa ajili ya wageni au wasomi, huku wakilenga wananchi wa kawaida mijini na vijijini.

Wanachanganya Kiingereza, huku baadhi yao wakiwa hawakijui, lakini wakiokoteza maneno ya lugha hiyo ya kigeni ili kujiridhisha, kuwa kufanya hivyo kunawaonyesha kuwa wasomi, lakini kumbe ni kujiaibisha na kukataa kilicho chao.

Hapana shaka kuwa, Profesa Kabudi anakijua sana Kiingereza pengine kuliko hata Kiswahili, lakini ameonekana pamoja na usomi wake, kuitetea lugha hiyo ambayo ni moja ya tunu za taifa hili, zilizounganisha Watanganyika katika kupigania uhuru wao.

Pia, ni alama ya utambulisho kwao wawapo na watu wa mataifa mengine, mbali tu na kujivunia kuwa waasisi na mabingwa wa lugha hiyo duniani, hata kuvutia mataifa mengine kuizungumza na kutaka kufundisha watu wao.

Kama alivyoshauri Profesa, ni vizuri sasa wizara hiyo pamoja na ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kufanya kila liwezekanalo kuhakikisha shule zinagawiwa kamusi za Kiswahili, ili kuisaidia kujifunza na kufundisha Lugha hiyo kwa kizazi kichopo.

Lakini yote haya yanahitaji kujitolea, lakini pia dhamira ya dhati ya kuhakikisha linafanyika hili badala ya kuishia bungeni, baada ya hotuba kujadiliwa na kupitishwa na kufuatiwa na mchapalo wa kupongezana na hatimaye mambo kubaki kama kawaida, Kiswahili kikiendelea kusiginwa.

UCHUMI

# RC awafuata wakulima shambani kuweka sawa dai 'pamba halilipi'

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

• Nao wamwanikia kilichojificha moyoni...

KWA miaka mingi wakulima zao la pamba wamekuwa wakilalamika bei yake iko chini, hivyo kuwafanya kushindwa kuinuka kiuchumi na kubaki kuwa maskini.

Hadi sasa kisera, bei ya zao hilo linapangwa na Soko la Dunia na kisha serikali nchini hutangaza bei elekezi ya ununuzi, ambayo katika msimu wa kilimo uliopo sasa, ilitangazwa Sh.1,150 kwa kilo moja.

Kutokana na madai bei hiyo ya ununuzi siyo rafiki kwa mkulima, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Anamringi Macha, ameamua kufanya ziara kwa wakulima kuwasikiliza na kutoa elimu ya kinachopaswa kufanyika katika msimu ujao wa kilimo, 2024/2025, wasilime kimazoea, bali walime kisasa.

Mkuu wa Mkoa - Macha, anawaambia wakulima kwamba, bei siyo tatizo sana, shida ni namna ya ulimaji anaouita 'wa kimazoea' hivyo anawataka kuhamia katika kilimo chenye tija na kisasa, ambacho kunalimwa shamba dogo, lenye mavuno mengi.

Anasema mkulima anapolima kimazoea, wastani wa ekari moja, ni lazima apate wastani wa kilo 200.

Hapo Mkuu wa Mkoa analinganisha kinyume chake kwamba, mkulima akifuata ushauri wa maofisa ugani, ni wazi katika kila ekari moja anaweza kupata kilo 1,800 hadi 2,000, ambazo anazitaja ni zenye faida.

"Mfano ekari moja ya pamba umelima kisasa na kugharamia Sh. 260,000 na ukapata mavuno kilo 1,800 na ukauza kwa Bei ya sasa ya Sh.1,150 kwa kilo, utapata Sh. milioni 4.1, tayari utakuwa na faida, tofauti na kulima kimazoea ambayo kwa kilo 200 utapata Sh.230,000 na kupata hasara ya Sh.30,000 au zaidi," anasema Macha.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Anamringi Macha akisaidia wakulima wa pamba wilayani Kishapu, kuiweka kwenye mizani. **PICHA: MARCO MADUHU**

Anawashauri wakulima kwamba, katika msimu ujao wa kilimo, 2024/2025, wakulima wanatakiwa kuwatumia vyema maofisa ugani kulima kisasa, pamoja na maofisa hao nao wawatembelee wakulima na kuwapatia elimu.

Mkuu wa Mkoa anasisitiza kwamba, wataalamu kilimo hao kwa sasa wana usafiri wa pikipiki waliopewa na serikali, ili wazunguke kuwafikia wakulima wakawabadilishe na kukifanya kilimo kiwe chenye tija.

"Nilivyoapishwa na Rais Samia kuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, moja ya majukumu ambayo nilipewa ni kusimamia zao la pamba.

"Nimekuja katikati ya msimu na sasa ni kipindi cha mavuno. Msimu ujao nitakuwa nanyi bega kwa bega, hakuna tena kulima kimazoea. Maofisa ugani orodhesheni majina yote ya wakulima wa pamba," anasisitiza Macha.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba Tanzania Marco Mtunga, anatilia makazo kwa kauli kwamba wakulima wengi wa pamba hasa wilayani Kishapu, bado wanapenda kulima kimazoea kwa kumwaga mbegu shambani, badala kufuata kanuni za kilimo kwa kuzipanda kwa mstari, ili wapate mavuno mengi.

Anawasisitiza wakulima, pia wazingatie ubora wa pamba wanayozalisha, pamoja na kuepuka kuichafua kwa kuweka maji, mchanga ninapokwenda kuiuza, ili kutosababisha kushuka thamani ya zao hilo katika soko la nje na kufanya bei kuwa chini.

### WAKULIMA WANENAVYO

Mkulima James Ally kutoka Kijiji cha Shagihilu wilayani Kishapu, analalamika kwamba hadi sasa bei elekezi ya pamba iliyotolewa na serikali, bado haimtoi mkulima kwenye umaskini.

"Ukilima ekari moja ya pamba tangu maandalizi ya shamba, hadi kuvuna huwa tunatumia zaidi ya Sh. 260,000 na kilimo chetu cha mazoea ekari hiyo moja, unatoa kilo 200 za pamba.

"Sasa ukiuza kwa Sh.1,150 kwa kilo, unapata Sh. 230,000 hapo tayari una hasara ya Sh. 30,000 na bado kuna gharama zingine tumeziacha," anasema Ally.

Mwananchi mwingine, Nicodemas Masesa, masikitiko yake kwamba, anachodai "zao la pamba kutopewa hadhi yake kama mazao mengine likiwamo la Tumbaku,", ambalo kila msimu bei yake huwa inapanda, lakini kwa pamba inashuka.

"Wakulima wengi wameshaachana na kilimo cha zao la pamba, kwa sababu halimtoi kwenye umaskini. Tumebaki sisi ving'ang'anizi... wenzetu waliolima mpunga wako vizuri kiuchumi, sababu ya bei kuwa nzuri," anasema Masesa.

Mwananchi John Idoto, ana ushauri kwamba ili bei ya pamba iwe nzuri, ni vyema serikali ikafufua viwanda vilivyokufa vya kutengeneza nguo zitokanazo na pamba nchini.

## Dk. Samia akanyaga Korea Kusini, akitarajiwa kurejea na mazito matatu

**INATOKA UK.11**

Hapo kunazugumziwa maeneo ya mbegu bora na teknolojia ya kisasa ya kilimo, huku kukiombwa ushirikano wa kitaalamu katika utekelezaji wa Programu ya Vijana – BBT (Building a Better Tomorrow).

Yun Jongchul, Makamu Mtawala Mkuu wa KOPIA anampongeza Rais Dk. Samia Suluhu, kwa utashi wake kukuza kilimo kwa kuiongezea bajeti, naye akiahidi wao KOPIA, wako tayari kushirikiana na kuanzisha kituo chao nchini, kukuza utafiti kilimo na matumizi ya teknolojia kisasa, hasa kwa BBT.

Balozi wa Tanzania nchini Korea Kusini, Togolani Mavura, akaishukuru taasisi ya KOPIA kwa utayari wake kufanya kazi na Tanzania, akiahidi kusimamia makubaliano hayo ya kuanzishw kituo hicho, ikiwa ni sehemu ya kutekekeleza ajenda ya kilimo Tanzania.

Ni katika mwendeleo wa ishara kama hiyo, Waziri Mkuu akakutana na ujumbe kutoka Korea Kusini, Septemba mwaka jana, kujadili mikakati ya ushirikiano wa maendeleo kwa pamoja.

Ni sura ya ushirikoano inayorejea tena Januri mwaka huu, pale Waziri wa Nchi Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, akisema jijini Dodoma kwamba, ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na Korea Kusini umechochea kwa kiasi kikubwa utekelezaj wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini, ikiwamo mradi wa kimkakati wa daraja la Tanzanite, Dar es Salaam, lililojengwa kwa ufadhili wa serikali ya Korea Kusini, kupitia Mfuko wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kiuchumi (EDCF).

Ilikuwa kauli yake waziri, wakati wa kutia saini makubaliano yaliyohusisha Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi ya National Agency for Adminstrative City Construction and Heerim Architects and Planners ya nchini Korea Kusini, ikisanifu na ujenzi nchini wa majengo na miundombinu, jijini Dodoma.

Hapo akarejea uhusiano huo unadhihirishwa pia na ziara za viongozi wa ngazi ya juu (wakati huo) katika mataifa hayo mawili; moja ilifanywa Oktoba 2022, kwa ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa.

"Akiwa Korea Kusini Mheshimiwa Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) aliitembelea National Agency for Administrative City Construction. Taasisi hii ni wakala wa kitaifa nchini Korea Kusini inayosimamia na kuendeleza ujenzi wa jiji la Sejong nchini humo.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa niaba ya Serikali ya Tanzania kumkaribisha Mtendaji Mkuu wa taasisi hii Nchini Tanzania ili kubadilishana uzoefu na viongozi wa taasisi zinazofanana na hizi hapa kwetu Tanzania," akasema Waziri Jenista

Miezi minne baadaye, nako kukashuhudiwa Chemba ya Biashara Viwanda na kilimo Tanzania (TCCIA) na wanachama wake, wakishuhudiwa wanashiriki Mkutano wa Kibiashara nchini Korea Kusini.

Kwa maana hiyo, ziara ya Rais Dk. Samia, ambayo inaendana na kuingia mikataba zaidi ya saba,vilevile zinailetea nchi fedha za maendeleo Sh.trilion 6.5.



# Waziri ahimiza uboreshaji maabara hospitalini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel amesema pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika sekta ya afya nchini, endapo maabara hazitaboreshwa uwekezaji huo hautakuwa na tija kwa taifa.

Dk. Mollel alisema hayo juzi jijini hapa kwenye mkutano wa wataalam wa maabara nchini ulifanyika kwa siku moja.

Alisema pamoja serikali kuwekeza kwenye ujenzi wa hospitali, vituo vya afya pamoja na zahanati kama maabara hazitaboreshwa bado wananachi wataendelea kulalamikia huduma mbovu za kimatibabu zinazotolewa nchini.

"Maabara ndiyo kila kitu katika sekta ya afya kama mgonjwa atapata vipimo ambavyo vitabainisha ugonjwa unaomsumbua na kuandikiwa dawa na kupona mara moja, basi hospitali hiyo itapata watu wengi lakini kama watu wanataka vipimo lakini majibu wanayopata siyo sahihi basi wagonjwa watapoteza imani na hospitali hospitali hiyo.

"Kwa maana hiyo basi tunapaswa kuwekeza kwenye maabara ili kuboresha huduma zetu za kimatibabu, hivi sasa watu wanakwenda kupata matibabu nje ya nchi hii yote ni kutokana na vipimo vyetu kuwa na changamoto, lakini kama tutawekeza kwenye maabara watu hawa hawataenda nje tena kufuta huduma za kimatibabu"alisema.

Aidha, alipongeza wataalamu wa maabara nchini ambao wamekuwa msaada mkubwa katika kuboresha huduma za kimatibabu kwa kutoa majibu sahihi ya vipimo vya magonjwa mbalimbali kwa wananchi.

Mkurugenzi wa Idara ya Ubora na Uchunguzi wa Magonjwa na Matengenezo ya vifaa tiba, Dk Alex Magesa alisema lengo la mkutano huo ni kutoa tuzo na vyeti kwa maabara zilizopata ithibati za kimataifa kwa mwaka wa fedha 2023-2024.


Alisema wadau wa maabara wanashirikana katika kuboresha sekta ya maabara lengo likiwa ni kuhakikisha huduma bora na nzuri zinatolewa.

Dk. Magesa alisema kwa sasa wana wadau wengi katika sekta ya maabara ambao mentali wapo 60 na wakaguzi 37.

Alitaja mafanikio yaliyopatikana mpaka sasa ni pamoja na kujenga uwezo wa maabara ya taifa na kuweza kugundua magonjwa ya milipuko kama mkoani Kagera.

Alisema hadi sasa wamefanikiwa kufikia maabara 83 ambazo zimepata idhibati ya kimataifa ambapo hali hiyo inaifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu yenye ithibati nyingi.

Kadhalika, alisema kupata ithibati ni gharama kubwa hivyo wanaishukuru serikali kwa kuweza kulisimamia jambo hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimwer, akisalimiana na wanafunzi wa shule ya msingi ya mchepuo wa kiingereza ya 'Dodoma English medium', alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya shule hiyo, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Singida wapewa elimu matumizi huduma za fedha

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Fedha imeanza kutoa elimu kwa wananchi wa Manispaa ya Singida ili wapate uelewe wa matumizi bora ya huduma za fedha, kujikwamua kiuchumi.

Ofisa Usimamizi Fedha kutoka Wizara ya Afya, Salim Kimaro, akizungunza jana alisema mafunzo hayo yatatolewa katika mikoa ambao ni mpango wa miaka mitano na yanatolewa kwa wajasiriamali, wanavikundi, vijana na wananchi wengine.

Kimaro alisema mpango wa Wizara ya Fedha katika utoaji wa elimu hiyo ni kuwafikia wananchi wa hali zote ili kuhakikisha wanafanikiwa kujikwamua kiuchumi.

Alisema utoaji wa elimu ya fedha umetokana na uwepo wa changamoto nyingi za wananchi kuingia kwenye mikopo bila uelewe na wengi wamekuwa hawajui ni wapi waweze kuwekeza fedha zao au watatumiaje fedha zao mara baada ya kustaafu.

"Wananchi hawana uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya fedha na hivyo kusababisha kupata changamoto nyingi ikiwemo kuomba mikopo kupitia taasisi zisizo rasmi ambazo wanaposhindwa kulipa mikopo husika taasisi hizo hutaifisha mali zao," alisema.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, alisema serikali inathamini wafanyabiashara ndiyo maana imekuwa ikipambana na changamoto ambazo zimekuwa zikiwakabili kwa kuhakikisha kila kitu kinaenda sawa.

"Serikali inawathamini wafanyabiashara na watanzania kwa ujumla ndiyo maana unaona hata upande wa elimu ni bure na hilo wengi mnalitambua, lakini hizo zote ni jitihada za serikali yetu," alisema.

Nao wafanyabiashara wao wamelalamikia kuwa bado tozo zimekuwa nyingi na zimekuwa zikilipwa kwa nyakati tofauti jambo ambalo wameiomba serikali ilirekebishe.

# Katibu TAMISEMI atoa maagizo walimu msingi, sekondari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Charles Msonde amesema walimu wa shule za msingi na sekondari wanapaswa kuwa karibu na wanafunzi ili kubaini kero zinazowasibu.

Alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na walimu wa shule za msingi na sekondari za Jiji la Dodoma kwenye kikao kazi cha kuwakumbusha majukumu yao.

Alisema walimu hao wanapaswa kuwa karibu na wanafunzi wao ili kutambua kero zinazowakabili na kuzifanyia kazi ili kuongeza ufaulu katika maeneo yao.

Alisema serikali inatambua na kuthamini mchango wa walimu katika kuleta maendeleo nchini, ndio maana imeamua kushughulia kero ambazo zilikuwa zikiwakabili ikiwemo za kuchelewa kupandishwa madaraja na stahiki za fedha za likizo.

Dk. Msonde alisema kutokana na dhamira ya dhati ya serikali katika kujali maslahi ya walimu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa aliagiza kuwa ikifika Julai hataki kusikia tena kero zinazohusu kuchelewa kupandishwa madaraja kwa walimu.

Aliongeza kuwa walimu wanafanya kazi kubwa ya kulea na kuwapa ujuzi watu mbalimbali ambao hatimaye unawasaidia wao binafsi kupata maendeleo na taifa.

Akizungumzia masuala ya mawasiliano, aliwaasa viongozi mbalimbali kuhakikisha wanapopokea barua, ujumbe na simu kutoka kwa wanaowatumikia kuhakikisha wanawajibu haraka na kupokea ushauri unaolenga kuboresha utoaji huduma kwa walimu.

Dk. Msonde aliwataka walimu wenye changamoto kupitishia kwa maofisa elimu wa shule za msingi na sekondari akisema wao ndio wanapaswa kupeleka barua na vielelezo vya walimu kwa maofisa utumishi ili kuepuka kupata majibu yanayowakatisha tamaa.

Pia, aliwataka walimu hao kuacha tabia ya kufanya kazi kwa mazoea, badala yake wanatakiwa kutoa elimu kwa ubunifu na kuwaacha kuwakatisha tamaa wanafunzi hata katika masomo ambayo wanadhani kuwa ni magumu.

0000000



# Lumbesa lawatesa wakulima wa viazi Isuto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa viazi Kata ya Isuto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kudhibiti vipimo visivyo rasimi ambavyo baadhi ya wafanyabiashara wanavitumia kuwanyonya ikiwemo ujazo uliozidi maarufu kwa jina la 'lumbesa'.

Walitoa malalamiko hayo juzi kwenye mkutano maalumu wa kusikiliza kero za vijana ulioitishwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Taifa (NEC), Ndele Mwaselela.

Mmoja wa wakulima hao, Stephano Shila alisema wanunuzi wa viazi wamekuwa wakienda na mifuko ambayo ni mikubwa kuliko waliyoizoea na kuwalazimisha wajaze ndipo wawauzie huku wakijipangia bei.

Alisema pamoja na kwamba mifuko wanayokwenda nayo huwa ni mikubwa, bado huwa wanajaza lumbesa hali ambayo inawasababishia wakulima hasara.

"Tunatumia nguvu na gharama kubwa kwenye uzalishaji lakini hawa wanunuzi wakija wanajaza lumbesa, serikali ilikataza vipimo vya aina hii lakini bado baadhi ya wanunuzi wa viazi wanaitumia," alisema Shila.

Naye Mussa Mwazembe aliumuomba Mwaselela awasaidie wakulima wa eneo hilo kuunda umoja ambao utakuwa unasimamia uuzaji wa viazi vyao na kupunguza baadhi ya tabia za kinyonyaji ikiwemo lumbesa.

Alisema wakiunda umoja huo wanaweza wakawa na nguvu kuliko sasa hivi ambapo kila mmoja anauza viazi vyake kulingana na mteja anayekuwa amempata.

Alisema viazi ni zao ambalo linaoza haraka endapo vitavunwa na kuhifadhiwa kwa hiyo vinahitaji kuuzwa haraka baada ya kuvunwa na hivyo endapo wakikataa kuwauzia wafanyabiashara wanaotaka lumbesa vinaanza kuoza.

Alisema kilimo cha viazi kwa sasa kina gharama kubwa kutokana na kuhitaji mbolea na dawa nyingi kuanzia kwenye kupanda mpaka kukomaa na hivyo wanahitaji kusaidiwa kuwakabili wanyonyaji.

Akijibu hoja hiyo, Mwaselela alisema chama hicho kitawaagiza viongozi wa serikali akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kushughulikia tatizo hilo.

Alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alishaagiza wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kushughulikia tatizo hilo ili wakulima wasiendelee kuumizwa na wanunuzi.

Alisema serikali kwa sasa imeweka mkazo mkubwa kwenye kuwasaidia wakulima na kwamba ndiyo sababu iliamua kuweka ruzuku kwenye mbolea ili wakulima wasitumie gharama kubwa kwenye uzalishaji.

Mwaselela alisema: "Hili nawahakikishia kwamba tutalishughulikia ndani ya muda mfupi ujao na mtapata taarifa, serikali kwa sasa inapambana kuboresha sekta hii ili taifa lijitosheleze kwa chakula na ziada iuzwe nje ya nchi"




Meneja wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Deusdedit Hokororo (kushoto), akizungumza na wananchi waliotembelea banda la kituo hicho, wakati wa maonyesho ya biashara mkoani Mbeya juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mama Samia Legal Aid yatatua mashauri ya muda mrefu

**Na Ibrahim Joseph,** NJOMBE

MKURUNGENZI wa Mashtaka Nchini (DPP), Silvester Mwakitalu amesema kupitia kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia wamefanikiwa kubaini na kutatua mashauri yaliyochukua muda mrefu mahakamani.

Mwakitalu alisema hayo juzi wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa akiwa kwenye kampeni ya Mama Samia ya msaada wa huduma za kisheria

Alisema kupitia kampeni hiyo ofisi ya DPP ilifanikiwa kupokea malalamiko ya baadhi ya wananchi kuhusu mashauri yao kucheleweshwa mahakamani

Mwakitalu alibainisha kuwa ofisi yake imekuwa ikichukua hatua ya kuyatatua mashauri hayo ambayo yamekaa kwa muda mrefu.

Alisema ofisi hiyo imekabidhiwa jukumu la kuratibu upelelezi kuyasajili mashtaka yote hapa nchini.

Pia, aliongeza kuwa kupitia kampeni hiyo malalamiko hayo yanashughulikiwa kwa kuagiza mamlaka kuzishughulikia kwa haraka.

Aidha, alisema ofisi hiyo imeshiriki kampeni hiyo na wamekuwa wakipita maeneo ya vizuizi ili kusikiliza kero za wafungwa na mahabusu waliopo huko .

Alisema ofisi yake katika kusogeza huduma karibu na wananchi mpaka sasa wanaofisi katika wilaya 62 na wataendelea kufungua maeneo mengine kulingana na bajeti.

Wakili Mkuu wa Serikali Wizara ya Katiba na Sheria, Lawrant Kabigi akitoa elimu kwa nyakati tofauti kwa wananchi wa Kijiji cha Nundu na Takubi aliwaomba wananchi kujenga tabia ya kuandika wosia ili kupunguza migogoro baada ya Mtu kufariki.

Kabigi alisema katika kampeni hiyo wamekuwa wakipokea malalamiko ya mirathi kucheleweshwa hiyo inatokana na wahusika kushindwa kuandika wosia.

Alitaja migogoro mingine ambayo wamekuwa wakikutana nayo ni migogoro ya ndoa na ardhi.

# Watakiwa kubuni mbinu kudhibiti maambukizi VVU

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SERIKALI ya Mkoa wa Mbeya imewataka wadau wa afya kufanya utafiti wa hali ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) mkoani hapa kubaini ufanisi wa mbinu zinazotumika kudhibiti maambukizi mapya na kubuni mbinu nyingine za kudhibiti.

Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye kikao kazi cha wadau kilicholenga kufanya tathimini ya ripoti ya utafiti uliofanyika mwaka 2022 kuonyesha bado kuna watu wanaishi na maambukizi bila kujitambua.

Homera, alisema taarifa ya utafiti huo inaonyesha kuwa kiwango cha maambukizi katika mkoa huo ni asilimia 9.6 na unashika nafasi ya tatu kitaifa baada ya Njombe na Iringa ambayo ni ya kwanza na ya pili.

Alisema 95 tatu za udhibiti wa maambukizi hayo, zinaonyesha kuwa ya kwanza ambayo inalenga kuhakikisha asilimia 95 ya watu wanaoishi na maambukizi hayo wajue hali ya maambukizi mafanikio yake ni madogo.

Alisema utafiti huo wa 2022/2023 unaonyesha asilimia 91 pekee ya watu wanaoishi na maambukizi hayo wanazijua hali zao na kwamba takwimu hizo zinatia wasiwasi kuwa juhudi za wadau bado hazijazaa matunda.

Homera, aliwataka wadau kufanya utafiti ili kupata takwimu zenye uhalisia kwa maelezo kuwa wananchi wengi kwa sasa wanajitambua na wanajilinda hali ambayo ilitakiwa kiwango cha maambukizi kishuke.

"Lazima tutumie mbinu tulizozitumia kwenye masuala ya udumavu na ukondefu kupunguza takwimu hizi, kwahiyo nawaomba TACAIDS na wadau wengine mfanye utafiti upya maana kila mwaka tunaonekana tumefikia asilimia 91, ina maana hizi kazi zote za wadau zinaonekana hazisaidii," alisema Homera.

Aliwataka wadau kushirikiana na halmashauri kufanya tathimini za ndani ili kubaini hali ilivyo na kuongeza mbinu zaidi za kudhibiti maambukizi.

Mratibu wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Petro, aliahidi kushirikiana na viongozi wa Mkoa wa Mbeya kufanya utafiti ili kupata takwimu zenye uhalisia.

Petro, alisema watashirikisha na taasisi iliyofanya utafiti wa mwaka 2022/2023 ili kupata viashiria vingine vya maambukizi ambavyo ilibaini ili na wao wavitumie kufuatilia.

Alisema viashiria watakavyohitaji ni vile vinavyoonyesha hali ilivyo kwenye halmashauri ambako ndiko takwimu hizo zilianzia kukusanywa.

"Ikiwezekana tutamwandikia barua Mtakwimu Mkuu wa Serikali atusaidie kuchakata takwimu zote tunazozihitaji ili tujue ukubwa wa tatizo na namna ya kukabiliana nalo," alisema Petro.

Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo inakabiliwa na takwimu za juu za maambukizi ya VVU kutokana na mwingiliano mkubwa wa watu kutokana na kupitiwa na barabara kuu ya kwenda nchi za Zambia na Malawi.

# Waziri: Toeni taarifa mkipewa huduma mbovu hospitalini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imewataka wananchi wanaofika katika hospitali za serikali wasisite kutoa taarifa endapo hawataridhishwa na huduma walizopewa ili hatua za kinidhamu zichukuliwe.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh aliyasema hayo wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Nungwi, Abdallah Abasi Wadi aliyehoji kwamba bado yako malalamiko yanayohusiana na manyanyaso wanayoyapata wananchi.

Akijibu swali hilo, Hassan alisema wizara yake imekuwa ikichukua hatua kadhaa za kiutumishi kwa watumishi wanaoendana kinyume na utaratibu wa kazi. Alisema lengo kuu la Wizara kupitia watendaji wake ni kutoa huduma bora na stahiki kwa wananchi wote bila ya ubaguzi na katika kuboresha utoaji wa huduma za afya. Katika hatua nyingine akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Wingwi, Kombo Mwinyi Shehe aliyetaka kujua kwa kiasi gani mfumo unaorahisisha taarifa za mgonjwa kuweza kusomeka na kufahamika katika kila eneo la hospitali husika kwa kiasi gani umeweza kurahisisha upatikanaji wa huduma kulingana na dhamira iliyokusudiwa.

Naibu waziri huyo alisema wizara imeanzisha mfumo unaorahisisha taarifa za mgonjwa kuweza kusomeka na kufahamika katika kila eneo la hospitali husika kutoka mapokezi hadi kwenye eneo la dawa.

Alisema mfumo huo umeanza kwa hatua za majaribio katika baadhi ya hospitali na vituo vya afya ikiwemo Makunduchi, Kitogani, Kivunge, Chakechake, Micheweni, vitongoji, Abdalla Mzee na Rahaleo.

Alisema lengo ni kubaini changamoto zinazojitokeza na kuzifanyia kazi kabla kuanza kuutumia rasmi katika vituo vyote Ungjua na Pemba.

Aidha, alisema wastani wa watendaji 50 kutoka katika kila kituo cha afya na hospitali husika wamepatiwa mafunzo ili kuweza kuendana na lengo lililokusudiwa.

# Alalamika mizigo kukaguliwa na mbwa bandarini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Mtabwe, Dk. Mohammed Ali Suleiman amesema kumekuwa na kadhia katika Bandari ya Dar es Salaam kwa muda mrefu kwa wasafiri wanaosafiri na meli za usiku kwenda Zanzibar.

Amesema wasafiri wengi wamekuwa wakipekuliwa mizigo yao kwa kutumia mbwa, kitendo ambacho ni kinyume na imani za wananchi wengi.

Alitoa malalamiko hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi katika kipindi cha maswali na majibu.

Alisema jambo hilo limekuwa likilalamikiwa na wasafiri wengi kwamba linawadhalilisha na kuwaweka katika wakati mgumu kwa mujibu wa imani zao.

"Je, serikali inalitambua tatizo hili na ni hatua gani imechukua kulitatua ili kuepusha taharuki kwa wasafiri" alihoji mwakilishi huyo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadil Abdulatif alisema ni kweli kumekuwa na ukaguzi wa kutumia mbwa katika Bandari ya Dar es Salaam kwa wasafiri wanaosafiria meli za usiku kuja Zanzibar kutokana na usalama kwa wakati huo kupitia meli za mizigo.

Alisema serikali inalitambua suala hilo akisema mamlaka zinazohusika na ukaguzi hutumia mbwa kwa ajili ya mizigo tu kwa lengo la kupambana na uingiaji wa dawa za kulevywa pamoja na kudhibiti uingizaji wa bidhaa haramu nchini.

Hata hivyo, alisema mamlaka za bandari kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi kwa pamoja wanaendelea na hatua mbalimbali za kuweka njia mbadala ambazo zinatumika kufanya ukaguzi kwa ufanisi zaidi bila ya kutumia mbwa kwa lengo la kuwaondoshea usumbufu huo wananchi wanaosafiri na meli za usiku.

"Utaratibu wa mizigo inayoingia Zanzibar kupitia Bandari ya Dar es salaam ni kwamba hukaguliwa kupitia mashine zilizopo bandarini.

Ili kuepusha malalamiko kama hayo kwa upande wa Zanzibar, Shirika lina mpango wa kuleta x-ray za kisasa zenye mfumo wa akili bandia zitakazosaidia wakaguzi kutambua dawa za kulevya pamoja na vihatarishi vingine" alisema Nadil.

Aidha, alisema Mamlaka ya Bandari za Tanzania (TPA) inafanya kazi zake chini Wizara ya Uchukuzi Tanzania Bara ambapo Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar anasimamia Mamlaka ya Bandari Zanzibar.

Alisema Wizara zinazohusiana na masuala ya bandari zinaendesha na kufanikisha kazi zao kupitia vikao vya pamoja vya ushirikiano.

Alisema vikao hivyo hufanyika kila baada ya robo mbili katika mwaka na kuhusu uhakika wa kuweka mashine ya kuchunguza mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam kupitia TPA aliahidi kuwaomba maofisa wa Tanzania Bara kulifanyia kazi kwa haraka kwa lengo la kuwaondoshea usumbufu wasafiri.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Balozi wa Norway nchini, Toni Tinnes alipofika Ikulu, jijini Zanzibar jana kwa mazungumzo na kujitambulisha. **PICHA: IKULU**

# Makamu wa Rais ataja faida Makumbusho ya Amani

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amesema Makumbusho ya Amani na Viumbe Hai yatasaidia katika kukuza sekta ya utalii na uchumi wa nchi.

Aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa makumbusho hayo yaliyopo Mnazi Mmoja mjini Zanzibar.

Alisema serikali imejipanga kufanya ukarabati katika maeneo yote ya kihistoria ikiwemo eneo Fufuni Pemba, Msikiti wa Kichokochwe Pemba, eneo la kihistoria la Maruhubi pamoja na Mahamamu ya Forodhani, Kijichi, Hamamni na Kizimkazi Unguja kwa lengo la kukuza sekta ya utalii pamoja kuengeza pato la nchi.

Hemed alisema kuwa serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale itaendelea kuyaendeleza maeneo ya kihistoria kwa kuzungusha ukuta, uwekaji wa vitu vya kale, kuyajenga ili kurudisha uasili wake sambamba na kuimarisha majengo ya utoaji wa huduma kama vile vyoo, migahawa na maduka.

Alisema kwa kutambua na kuthamini umuhimu mkubwa wa makumbusho, ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 imechukua hatua ya kuweka mazingira mazuri katika maeneo ya makumbusho kwa kutunga Sheria ya Uhifadhi wa Mambo ya Kale Namba 11 ya Mwaka 2022 inayosimamia kutunza, kuhifadhi na kuendeleza makumbusho ya mambo ya kale.

Aidha, aliwataka wafanyakazi wa Makumbusho ya Amani na Viumbe Hai pamoja na makumbusho mengine kuendelea kuimarisha na kuyatunza ili yaendelee kuwa kivutio cha wageni wengi zaidi wa ndani na nje ya nchi.

Pia, aliitaka jamii kutokuyavamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya makumbusho ya historia na badala yake waendelee kushirikiana na serikali katika kuyalinda na kuyaimarisha.

Naye Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inahuwisha sekta ya utalii na mambo ya kale kwa kuyafungua makumbusho yote ambayo yalikuwa hayafanyi kazi ndani ya Zanzibar.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Utalii imejipanga katika kuyajenga na kuyafanyia ukarabati maeneo ya kihistoria na maeneo mengine ambayo ni vivutio vya watalii.

Katibu Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Dk. Aboud Suleiman Jumbe alisema kupitia mradi wa kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya urithi serikali imeamua kuyafanyia ukarabati na kuimarisha maonesho ya makumbusho ili kuyarejesha katika haiba yake.

Jumbe alisema kuwa makumbusho yana umuhimu mkubwa katika uimarishaji wa elimu na utafiti, kuchangia uimarishaji wa utalii wa ndani na nje katika kukuza uchumi wa nchi pamoja na kuhakikisha uhifadhi wa urithi wa kihistoria na kiutamaduni kwa vizazi vijavyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAIDA CHARLES MAJIRA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 0630-0033** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYEGINA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/86146/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JENIPHER RICHARD KIMANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha Diploma ya **CLINICAL MADICINE** Chenye **No. 0148181.** Kilichotolewa na **NACTVET** kupitia **CHUO CHA AFYA MVUMI** mwaka 2023, Cheti hiki kimepotea Jijini Dodoma. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/17816/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**ALLI AZIZI RASHID,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye NAMBA ZA USAJILI **MC733BZR,** CHASSIS namba **MD6M14PAX4E19273, ENGINE NAMBA AK4EJ4824156,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/19392/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NDG.JOSHUA DANIEL MGOGO** KWA NIBA YA **NDG.ALICE CYPRIAN MUSHI** ,ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA **T 424 ATY.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA ARIPOTI KWENYE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TARIFA YA POLISI
**PHQ/IR/MUF/5034/2024**

## KUBADILI JINA

Mimi Thulasee das Thekkepulippra Gopalan, S/o Marehemu shri Velu Gopalan, Raia wa India, mwenye hati ya kusafiria halali ya India **M-1470775** na pia mwenye kibali halali cha ukazi cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania namba **WPC64734/23** na **RPQB011867923A00** na 12 ya kudumu -B, Pocket C-II, Mayur Vihar Phase -III, New Delhi 110096, na kwa sasa naishi Dar Es salaam na kufanya kazi na M.M. Industries Ltd nimebadilisha jina langu kutoka Thulasee das Thekkepulippra Gopalan kwa **Thulasee Das T.G** hadi madhumuni yote yajayo.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 8200 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ANDREW PETRO SEMHAMBULE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY PETER ANDREA SEMHAMBULE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration Is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 28th day of June 2024

Dated at Korogwe this 30th day of May 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 11581 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**

**TURUFAINA ONESMO MSEMO.................MAREHEMU**

**HANS ONESMO MSEMO...........................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 04 Mwezi JUNI, Mwaka 2024.
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 30 Mwezi MEI Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 12449 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**

**PHILIP TIMOTH MSHANGA...........MAREHEMU**

**FILBAT PHILIPO MSHANGA.........MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 05 Mwezi JUNI, Mwaka 2024.
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 30 Mwezi MEI Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA DODOMA**

**RUFAA/MADAI NA.3547/2024**

**Katika Mahakama ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**KENEDY RICHARD TARIMO.......... MRUFANI**

**DHIDI YA**

**JANE WILLIAM LUKUTA.........MRUFANIWA**

**KWA: JANE WILLIAM LUKUTA**

Kwa Rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya JUMATATU tarehe 10/06/2024 unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamoja na vielelezo vyovyote kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 09 Mwezi 05 Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
DODOMA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 10524/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late SEBASTIAN FRANCIS LOBOKA of MAILIMBILI Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY REVOCATUS SEBASTIAN MSAFIRI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

..................................................

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of JUNE, 2024
Date at Dodoma this 10 Day of MAY, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya ushetu,** anatangaza kupotelewa na kadi za magari mawili aina ya **TOYOTA LANDCURUSER HARDTOP** zenye namba za usajili **SM. 9804 na SM. 8999.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **NML/RB/LOSS/2022.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 11659 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GABRIEL JACOB MUYA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JACOB GABRIEL MUYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule of 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration id made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 21st day of june 2024
Dated at Korogwe this **28th day of May 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 11733N OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the late JACKLINE VALERIAN NJAU**

**and**

**In the matter of Application for letters of administration by NELSON PROTAS KAIJAGE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **15 day of 07 2024**
Dated at DAR ES SALAAM this **21 day of 05, 2024**

Principal Resident Magistrate

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie,***
**+255 - 745 700 710.**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.


Kwa

## HABARI KIMATAIFA

# Jeshi Israel ladhibiti ukanda wa Philadelph

**TEL AVIV,** Israel

JESHI la Israel (IDF) limesema kuwa limechukua udhibiti wa eneo la kimkakati kwenye mpaka kati ya Gaza na nchi ya Misri, linalojulikana kama Philadelphi ambalo liko katika eneo la Rafah

Msemaji wa Kikosi cha Ulinzi cha Israel (IDF), Rear Admiral Hagari, alisema katika eneo hilo wamegundua mahandaki 20 yanayotokeza hadi Misri zinazotumiwa na Hamas kuingiza silaha ndani ya Gaza.

Televisheni ya Misri ilinukuu vyanzo vilivyokanusha hilo, na kusema Israel ilikuwa inajaribu kuhalalisha operesheni yake ya kijeshi katika mji huo wa kusini mwa Gaza.

Tangazo hilo linakuja wakati wa mvutano mkali umeibuka kati ya Misri na Israel kuhusu uhalali wa wanajeshi hao kuingia eneo hilo.

"Katika siku za hivi karibuni, wanajeshi wa IDF walianzisha udhibiti wa operesheni kwenye Ukanda wa Philadelphi, kwenye mpaka kati ya Misri na Rafah," msemaji huyo alisema Jumatano.

Alielezea ukanda huo ambao unaaminika kama uhai kwa Hamas, kwa kuingizia silaha mara kwa mara katika Ukanda wa Gaza".

Hagari baadaye alisema katika kikao na wanahabari kwamba asingeweza kuwa na uhakika kwamba njia zote zilivuka hadi Misri, gazeti la New York Times liliripoti.

Njia ya Philadelphi ni eneo la huru, ambalo lina upana wa mita 100 katika sehemu ambayo inapita pembeni ya Gaza kwenye mpaka na Misri wenye km 13.

Awali, Misri ilisema ilikuwa imeharibu njia za kuvuka mpaka huo na kuzuia magendo ya silaha. Chanzo kutoka nchini Misri, kilichonukuliwa na Al-Qahera News, kiliishutumu Israel kwa kutumia madai hayo kuhalalisha kuendelea na operesheni kwenye mji wa Palestina wa Rafah na kurefusha vita kwa malengo ya kisiasa.

Israel ilisisitiza kuwa ni lazima ichukue mji wa Rafah ili kupata ushindi katika vita vilivyochochewa na shambulio la Hamas dhidi ya nchi hiyo Oktoba 7, mwaka jana na kusababisha vifo vya watu 1200 na wengine 252 kuchukuliwa mateka.

Katika vita hivyo jumla ya watu 36,170 wameuawa Ukanda wa gaza, kulingana na wizara ya afya inayoongozwa na Hamas.

Mvutano kati ya Misri na Israel umeongezeka tangu majeshi ya Israel yachukue udhibiti wa upande wa Gaza wa mpaka wa Rafah wiki tatu zilizopita.

Mapema wiki hii, mwanajeshi wa Misri aliuawa katika tukio lililohusisha wanajeshi wa Misri na Israel katika eneo la mpaka karibu na Rafah.

Misri inawaunga mkono sana Wapalestina na imelaani kampeni ya kijeshi ya Israel katika Gaza na mauaji ya maelfu ya raia. **BBC**

# ANC, DA vyachuana uchaguzi A, Kusini

**PRETORIA,** Afrika Kusini

MATOKEO ya awali ya uchaguzi mkuu wa Afrika Kusini, yameanza kutolewa, huku Chama cha African National Congress (ANC) kikiongeza kwa asilimia chache.

Katika matokeo hayo, dalili inaonyesha kwamba vyama vya ANC na DA, vinachuakana kwa ukaribu kwa kuzoa viti vya wabunge.

Uchaguzi huo unaelezwa kuwa na ushindani zaidi nchini Afrika Kusini tangu kumalizika kwa ubaguzi wa rangi na Nelson Mandela, kuwa mwafrika wa kwanza kushika nafasi ya urais yaliyotangazwa kutoka kwa zaidi ya asilimia 11 ya wilaya zilizopiga kura yanaonyesha chama cha ANC kinaongoza kwa asilimia 43, ikifuatiwa na DA yenye asilimia 26.

Chama chenye msimamo mkali cha wakulima kinachoongozwa na Julius Malema (EFF) (pichani) na Umkhonto weSizwe (MK Party) cha Rais wa zamani Jacob Zuma vina karibu asilimia 8.

Matokeo ya mwisho yanatarajiwa kutangazwa mwishoni mwa wiki.

Kura za maoni zinaonyesha kuwa chama cha ANC kinaweza kupoteza wingi wake bungeni kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 30.

Chama cha ANC kimepoteza uungwaji mkono kutokana na hasira juu ya viwango vya juu vya rushwa, uhalifu na ukosefu wa ajira.

Lakini ni mapema sana kutabiri matokeo ya mwisho. Uchaguzi uliofanyika wa Alhamisi ulishuhudia misururu mirefu ya wapiga kura nje ya vituo vya kupigia kura hadi usiku wa manane kote nchini.

Kura zinaendelea kuhesabiwa baada ya uchaguzi wa hapo jana nchini Afrika Kusini.

Mistari mirefu ilikuwa nje ya vituo vya kupigia kura kote nchini.

Afisa mmoja wa uchaguzi mjini Johannesburg aliiambia BBC kuwa misururu hiyo inakumbusha uchaguzi wa kihistoria wa 1994, wakati watu weusi walipiga kura kwa mara ya kwanza, na kushuhudia Nelson Mandela kuwa rais. **BBC**


twiga cement
Heidelberg Materials

## TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

### AUDITED RESULTS FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2023

**CHAIRMAN'S STATEMENT**

Dear Shareholders,
Dear Employees, Dear Friends of the Twiga Cement family,

The year 2023 has been a good year for us in many ways. As the Chairman of the Board, I am privileged and honoured to present this statement on behalf of the Twiga Cement family and the Board of Directors.

I convey my sincere gratitude to all our employees and partners, especially our frontline workers who consistently demonstrate exceptional commitment to ensuring the safety of our people and maintaining the strong performance of our business operations. Notably, our teams have remained steadfast in tackling the challenge of climate transformation by implementing sustainable measures including the further developments of alternative fuel-feeding systems and utilizing alternative raw materials to reduce clinker incorporation, thus reducing our carbon footprint on the environment.

**Financial Performance**

TPCPLC achieved an operating profit of TZS 141.4 billion, a 2.3% increase over 2022, despite a 2.2% decline in turnover. This profit growth was driven by disciplined cost control measures, offsetting the reduced market demand.

Additionally, TPCPLC's cash flow performance remained strong compared to the previous year. This improvement was primarily a result of enhancements in working capital management.

**Dividend**

The Board remains focused on building shareholders' value and we are confident that by following our strategies, we will achieve this. The Board, therefore, proposed a dividend for 2023 of TZS 390 per share. This is planned to be paid in June 2024.

**Appreciation**

On behalf of the Board, I want to express sincere appreciation to all of TPCPLC's stakeholders. Despite the challenges we encountered during the year 2023, your unwavering trust and support were instrumental in our continued success.

Looking ahead, we are confident that TPCPLC will continue to thrive thanks to the ongoing support of our entire stakeholder community.

Hakan Gurdal
**Chairman of the Board**

### STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME

| | Notes | 2023 TZS '000 | 2022 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| Revenue from contracts with customers | 7 | 490,171,829 | 501,369,007 |
| Cost of sales | 9 | (330,443,277) | (334,905,005) |
| **Gross profit** | | **159,728,552** | **166,464,002** |
| Other operating income | 8 | 9,745,144 | 501,513 |
| Selling and marketing costs | 10 | (5,891,729) | (3,082,702) |
| Net (charge)/release of expected credit losses | 23 | (11) | 339,944 |
| Administrative costs | 11 | (29,440,015) | (25,111,509) |
| Other operating expenses | 14 | (1,504,148) | (2,727,675) |
| Net gain on foreign currency translation | 17 | 8,795,332 | 1,829,993 |
| **Operating Profit** | | **141,433,125** | **138,213,566** |
| Finance income | 15 | 3,092,852 | 3,139,579 |
| Finance costs | 16 | (1,051,474) | (1,255,581) |
| Finance income - net | | **2,041,378** | **1,883,998** |
| **Profit before tax** | | **143,474,503** | **140,097,564** |
| Income tax expense | 32 | (44,290,757) | (42,738,964) |
| **Profit for the year** | | **99,183,746** | **97,358,600** |
| **Other comprehensive income** | | | |
| *Items that will not be reclassified to profit or loss:* | | | |
| Re-measurement gain/(losses) on defined benefit plan | 29 | (278,660) | 448,834 |
| Income tax effect | 32 | 83,598 | (134,650) |
| **Other comprehensive income for the year** | | **(195,062)** | **314,184** |
| **Total comprehensive income for the year, net of tax** | | **98,988,684** | **97,672,784** |
| **Earnings per share** | | | |
| Basic and diluted earning per share (TZS) | 40 | 551 | 541 |

### STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY

| | Share Capital and Share Premium (Note 27) TZS '000 | Retained earnings TZS '000 | Total Equity TZS '000 |
|---|---|---|---|
| As at 01 January 2023 | 3,598,462 | 296,139,811 | 299,738,273 |
| Profit for the year | - | 99,183,746 | 99,183,746 |
| Other comprehensive income, net of tax | - | (195,062) | |
| **Transactions with owners in their capacity as owners:** | | | |
| Dividends declared (Note 37) | | (70,170,009) | (70,170,009) |
| | - | (70,170,009) | (70,170,009) |
| **As at 31 December 2023** | **3,598,462** | **324,958,486** | **328,752,010** |
| As at 01 January 2022 | 3,598,462 | 268,637,039 | 272,235,501 |
| Profit for the year | - | 97,358,600 | 97,358,600.00 |
| Other comprehensive income, net of tax | | 314,184 | |
| **Transactions with owners in their capacity as owners:** | | | |
| Dividends declared (Note 37) | | (70,170,012) | (70,170,012) |
| | - | (70,170,012) | (70,170,012) |
| **As at 31 December 2022** | **3,598,462** | **296,139,811** | **299,424,089** |

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION

| | Notes | 2023 TZS '000 | 2022 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Non-current assets** | | | |
| Property, plant and equipment | 18 | 135,386,743 | 142,330,100 |
| Intangible assets | 19 | 858,706 | 813,318 |
| Leasehold land | 20 | 953,083 | 980,929 |
| Right of use assets | 21 | 1,004,266 | 4,333,991 |
| Other non-current financial assets | 25 | 352,000 | 574,000 |
| | | **138,554,798** | **149,032,338** |
| **Current assets** | | | |
| Inventories | 22 | 91,459,061 | 85,992,920 |
| Trade receivables | 23 | 61,659,567 | 53,561,114 |
| Other short-term operating receivables | 24 | 19,652,739 | 24,193,735 |
| Current income tax recoverable | 32 | 2,450,612 | - |
| Other current financial assets | 25 | 540,000 | 600,000 |
| Cash and bank balances | 26 | 131,369,615 | 105,512,644 |
| | | **307,131,594** | **269,860,413** |
| **TOTAL ASSETS** | | **445,686,392** | **418,892,751** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | | |
| **Equity** | | | |
| Share capital | 27 | 3,598,462 | 3,598,462 |
| Retained earnings | | 324,958,486 | 296,139,811 |
| | | **328,556,948** | **299,738,273** |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Lease liabilities | 28 | 185,766 | 1,149,572 |
| Employment benefit obligations | 29 | 5,386,658 | 4,937,695 |
| Provision for quarry site restoration | 31 | 4,573,453 | 4,266,311 |
| Deferred income tax liability | 32 | 10,559,783 | 10,066,665 |
| | | **20,705,660** | **20,420,243** |
| **Current liabilities** | | | |
| Lease liabilities | 28 | 963,806 | 3,461,375 |
| Employment benefit obligations | 29 | 562,206 | 401,627 |
| Current income tax payable | 32 | - | 521,690 |
| Trade and other payables | 33(a) | 81,389,778 | 78,394,395 |
| Provisions | 33(b) | 10,583,245 | 13,049,775 |
| Dividend payable | 37 | 2,924,749 | 2,905,373 |
| | | **96,423,784** | **98,734,235** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | | **445,686,392** | **418,892,751** |

### STATEMENT OF CASH FLOWS

| | Notes | 2023 TZS '000 | 2022 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **Operating activities** | | | |
| Profit before tax | | 143,474,503 | 140,097,564 |
| *Adjustment to reconcile profit before tax to net cash flows:* | | | |
| Depreciation and amortisation | 12 | 21,818,849 | 20,645,407 |
| Interest expense | 16 | 1,051,474 | 1,255,581 |
| Interest income | 15 | (3,092,852) | (3,139,579) |
| Net unrealised exchange (gain)/loss | 17 | (7,386,138) | (801,765) |
| Net provision for obsolete inventories | 22 | 2,902,936 | 971,658 |
| (Decrease)/increase in site restoration provision | 31 | 307,142 | 1,833,770 |
| Post employment benefit provision- Service cost | 29 | 336,169 | 300,809 |
| (Decrease)/increase in other provisions | 33(b) | (2,466,530) | (280,104) |
| Expected credit losses for trade receivables | 23 | (11) | 339,944 |
| Gain on disposal of property, plant and equipment | 8 | (8,540,612) | - |
| *Cash flows before changes in working capital items* | | **148,404,930** | **161,223,285** |
| *Working capital adjustments:* | | | |
| Inventories | | (8,369,077) | (34,029,089) |
| Trade receivables | | (8,098,442) | (7,623,738) |
| Other short-term operating receivables | | 4,540,996 | (7,606,867) |
| Other financial assets | | 282,000 | 222,000 |
| Trade and other payables | | 2,995,383 | 8,112,674 |
| *Net working capital adjustments* | | **(8,649,140)** | **(40,925,020)** |
| Corporation tax paid | 32 | (46,686,343) | (43,932,977) |
| Payment to post employment benefit - Benefit payments | 29 | (519,139) | (264,659) |
| Interest received | 15 | 3,092,852 | 3,139,579 |
| **Net cash inflows from operating activities** | | **95,643,160** | **79,240,208** |
| **Investing activities** | | | |
| Proceeds from disposal of property, plant and equipment | 8 | 8,540,612 | - |
| Payment for capital works-in-progress and PPE | 18 | (11,563,308) | (14,611,038) |
| **Net cash flows used in investing activities** | | **(3,022,696)** | **(14,611,038)** |
| **Financing activities** | | | |
| Dividends paid | 37 | (70,150,633) | (70,113,109) |
| Payment of lease liabilities - principal | 28 | (3,461,375) | (3,273,027) |
| Payment of lease liabilities - interest | 28 | (537,623) | (810,519) |
| **Net cash flows used in financing activities** | | **(74,149,631)** | **(74,196,655)** |
| **Net increase/(decrease) in cash and cash equivalents** | | **18,470,833** | **(9,567,485)** |
| Net unrealised exchange gain/(loss) | | 7,386,138 | 801,765 |
| Cash and cash equivalents at 01 January | | 105,512,644 | 114,278,364 |
| **Cash and cash equivalent at 31 December** | | **131,369,615** | **105,512,644** |

# MSIMU MPYA MARATHON DODOMA WAZINDULIWA

**Na Faustine Feliciane**

MSIMU wa tano wa mbio maarufu za marathoni mkoani Dodoma umezinduliwa rasmi jana na kutangazwa mwaka huu kufanyika Julai 28 jijini humo.

**Lengo la mbio hizo zinazodhaminiwa na benki ya NBC ni kukusanya fedha ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi na kutoa ufadhili wa elimu kwa wanafunzi wanaosomea taaluma ya ukunga ili kuboresha afya ya mama wa mtoto.**

Hafla ya uzinduzi huo imefanyika jana jijini Dar es Salaam ikihusisha wadau mbalimbali wa mbio hizo wakiwemo wawakilishi kutoka Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Taasisi ya Benjamin Mkapa, wadau wa habari pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo wakiongozwa na Mkurugenzi wao wa Fedha, Waziri Barnabas.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Barnabas alisema kuelekea msimu wa tano wa mbio hizo benki hiyo inajivunia mafanikio makubwa iliyoyapata misimu iliyopita ikiwemo makusanyo ya zaidi ya Shilingi milioni 700 ambapo kati ya hizo Milioni 600 zilielekezwa katika mapambano ya dhidi ya Saratani ya shingo ya kizazi kupitia ORCI na ufadhili wa masomo kwa wakunga 100 kwa kushirikiana na Taasisi ya Benjamin Mkapa.

"Zaidi tumeweza kuchangia ukuaji wa mchezo wa riadha nchini ambapo kwa kushirikiana na wadau wetu mbalimbali, tumeweza kukusanya zaidi ya wakimbiaji 12,500 na hivyo kuongeza hamasa kwa mchezo wa raidha nchini, tumekuwa tukichangia kuchochea utalii na uchumi wa Mji Mkuu wa Dodoma kupitia idadi kubwa ya washiriki wanaoenda kwa ajili yakushiriki mbio hizi na pia tumewa kuzalisha vipato na ajira kwa vijana ambapo mpaka sasa tumetoa zaidi ya Shilingi Milioni 274 kama zawadi kwa washindi na hivyo kuchangia vipato vya familia," alisema Barnabas.

Akifafanua zaidi kuhusu maandalizi ya mbio hizo Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Tasiana Masimba alisema katika msimu wa tano wa mbio hizo benki hiyo imejipanga kuvutia washiriki 8,000 kutoka 5,000 walioshiriki msimu uliopita lengo likiwa ni kukusanya fedha kiasi cha Shilingi Milioni 300 ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

"Kupitia misimu iliyopita tayari tumefanikiwa kufadhili vipimo vya saratani (screening) ya wanawake 40,000 ambapo kati yao 1,600 waligundulika kuwa na vimelea vya saratani na wakaanza matibabu mapema. Kwa upande wa wakunga tunalenga kusomesha wakunga 500 ifikapo mwaka 2028 ambapo tayari 100 tumeanza nao msimu uliopita wa mbio hizi. Tunachoomba tu watanzania waendelee kutuunga mkono kwenye jitihada hizi muhimu kwa kujisajili kwa wingi," alisema Tasiana.

Aidha, aliwashukuru wadau wa mashirika na makampuni mbali mbali waliojitokeza kudhamini mbio hizo.

## Mashindano ya kuogelea walemavu kufanyika Dar

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya pili ya Taifa ya mchezo wa kuogelea kwa watu wenye ulemavu yanatarajiwa kufanyika Oktoba 12 mwaka huu kwenye bwawa la kuogelea la Klabu ya Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Lengo la mashindano hayo ni kuimarisha uwezo wa waogeleaji ili waweze kuonyesha ushindani katika michuano ya kimataifa.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha mchezo huo Tanzania (TPSA), Ramadhani Namkoveka alisema mashindano hayo yatahusisha waogeleaji wenye ulemavu wa akili, ngozi pamoja na macho.

"Lengo la mashindano hayo ni kutambua kuendeleza na kusaidia kuinua vipaji vya waogeleaji wa Tanzania katika harakati zao za kushindana kwenye mashindano ya Kitaifa na Kimataifa," alisema Namkoveka.



Watoto wakitumbuiza wakati wa fainali za michuano ya 'African Schools Football' zilizofanyika kwenye Uwanja wa Amaan Complex, Zanzibar hivi karibuni ambapo timu ya Tanzania iliibuka bingwa baada ya kuifunga timu ya Guinea bao 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## Mfaume amuonya Tony Rashid

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Mfaume Mfaume kutoka kambi ya Nacooz ya jijini Dar es salaam ametoa tambo na kumtisha bondia Tony Rashid ambaye anatarajia kupambana na Oscar Richard kutoka katika kambi hiyo.

Mabondia hao wanatarajia kupanda ulingoni Juni 29 katika pambano lililopewa jina la 'Dar Boxing Derby'.

Akizungumza na Nipashe jana, Mfaume, alisema wamejipanga vema kuhakikisha wanamchapa mpinzani wao huyo kama mtoto.

"Kwa upande wetu tutahakikisha tunamchapa mpinzani wetu ili ajue watoto wa mabibo hatutaki utani tukiwa kazini," alisema Mfaume.

Aidha aliwataka wadau wa ngumi wajitokeze kwa wingi siku hiyo wajionee burudani itakayokuwa inaonyeshwa na bondia wao.

Kwa upande wake Oscar Richard alisema hana hofu yoyote kukutana na mpinzani wake huyo kutokana na mazoezi anayoendelea kuyafanya.

"Kwa upande wangu nimejipanga vizuri kukutana na Tonny, ni bondia ambaye haniumizi kichwa hivyo ninaomba mashabiki wangu waje kwa wingi waone burudani nitakayoitoa, alisema Richard.

Mbali na pambano hilo vile vile kutakuwa na mapambano mengine likiwemo la Juma Choki dhidi ya Nassibu Ramadhani, huku Haidary Mchanjo akiumana na Charles Tondo.

## ZISIKUPITE

### BRANTHWAITE ANYATIWA

KLABU ya Manchester United inamyatia beki wa Everton mwenye miaka 21, Jarrad Branthwaite, ambaye thamani yake ni kati ya pauni milioni 60 hadi 70. ***(Sky Sports)***

### GALLAGHER ATAKIWA

KLABU ya Aston Villa inavutiwa na kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher mwenye miaka 24. (***Independent***)

### ZETTERER AWANIWA CITY

KLABU ya Manchester City inafikiria kumnunua mlinda mlango wa Werder Bremen Mjerumani mwenye miaka 28, Michael Zetterer. ***(Sport Witness)***

### BRADLEY MKATABA MPYA

LIVERPOOL inapanga kumpa mlinzi wa Ireland Kaskazini, Conor Bradley mwenye umri wa miaka 20, mkataba mpya ulioboreshwa. ***(Mail)***

### MASON KUBADILISHWA

KLABU ya Manchester United inazingatia mkataba wa kubadilishana unaohusisha mshambuliaji wa Uingereza Mason Greenwood mwenye miaka 22 na mshambuliaji wa Ureno na Atletico Madrid, Joao Felix mwenye miaka 24. ***(Star)***

### ESTEVE AWINDWA EPL

EVERTON na West Ham wameanza mazungumzo na Burnley kuhusu mpango wa kumnunua beki Mfaransa mwenye umri wa miaka 22 Maxime Esteve. ***(L'Equipe)***

### AITAKA LEICESTER

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Ruud van Nistelrooy mwenye miaka 47 anawania nafasi ya kuwa kocha wa Leicester. ***(Mirror)***

### MBAPPE RASMI REAL MADRID

REAL Madrid inapanga kutangaza usajili wa mshambuliaji wa Ufaransa na PSG, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 25, kabla ya michuano ya Euro msimu huu wa majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

### CHELSEA KUCHANGISHA

CHELSEA italazimika kuchangisha fedha kupitia mauzo ya wachezaji kabla ya Juni 30 ili kuzingatia kanuni za faida na uendelevu za Ligi Kuu ya England. ***(Sun)***

### ATAKA KAMPANI YAKE

KOCHA mpya wa Bayern Munich, Vincent Kompany anataka kocha wa Middlesbrough, Aaron Danks ajiunge na benchi lake la ufundi ndani ya klabu hiyo. ***(Mail)***

### FELIX KUREJEA BARCA

KLABU ya Barcelona huenda wakamrejesha Nou Camp kwa mara ya pili mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix kutoka Atletico Madrid. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GERRARD AFICHUA KUTAFUTA USHAURI KWA FERGUSON

**LONDON,** England

### ●●● Ni baada ya kutimuliwa katika nafasi ya ukocha kwenye klabu ya...

STEVEN Gerrard amefichua kwamba alimtembelea kocha wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson kwa ushauri baada ya kutimuliwa katika klabu ya Aston Villa.

**Kiungo huyo wa zamani wa Liverpool aliondolewa kwenye nafasi yake ya ukocha Oktoba 2022, huku Villa ikishinda michezo miwili pekee ya ligi na kuteleza kuelekea eneo la kushushwa daraja.**

Kufukuzwa kwake kulitoa mwanya kwa Unai Emery kujiunga na timu hiyo uteuzi ambao umewawezesha kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Gerrard amekiri kwamba kupoteza kazi yake ilikuwa "ngumu", na kumwacha akitafuta mawazo ya wengine.

Mtu mmoja aliyemfikia, alikuwa ni Ferguson na, katika mahojiano na Telegraph, Gerrard ameeleza kwa kina mazungumzo na ushauri alipokea.

Alisema: "Mimi sio mmoja wa watu wanaoonekana kuwa wa kulaumiwa, ambaye anaonekana kunyooshewa vidole. Sio mtindo wangu na ndio sababu nilihitaji muda wa kushughulikia ugumu huo, Ilipunguza ujasiri wangu kidogo.

"Nilizungumza na wasimamizi wengi. Nilienda kuonana na Alex Ferguson kwa saa kadhaa na akasema, 'Chukua muda wako, usirukie chochote. Chukua muda wako na ujichambue.'

"Na hivyo ndivyo nimefanya. Lakini haijaathiri azma yangu. Sikuwa na malengo yoyote nilipoanza safari hii tofauti. Sikuwa na mpango wa kwenda Glasgow Rangers.

"Sikuwa na Aston Villa kwenye wasifu wangu. Ninaendelea kujaribu kuwa toleo bora kwangu na kuwa na taaluma ya ukocha kwa sababu ninaipenda sana.

"Kutimuliwa na Villa ilikuwa ngumu. Iliniuma, lakini kile ambacho watu wanahitaji kuelewa ni kama sikuhisi hivyo, kama sikuchukua hilo kibinafsi, kama sikuwajibikia kikamilifu. Kwamba, basi mimi si Steven Gerrard tena kwa sababu wakati ni mpira wa miguu na ni wa kitaalamu na ni kitu ambacho ninakipenda, nitakimiliki daima."

Gerrard aliteuliwa kuwa kocha wa Al Ettifaq msimu wa kiangazi wa 2023 na kuiongoza klabu hiyo hadi nafasi ya sita kwenye Ligi ya Saudia katika msimu wake wa kwanza.

# MBAPPÉ: NATAMANI KUICHEZEA AC MILAN

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappé anatarajiwa kutimiza ndoto yake ya maisha na kujiunga na Real Madrid msimu huu wa majira ya joto, lakini fowadi huyo amesema angependa kuichezea AC Milan siku moja.

Mbappé alisema alikuwa shabiki mkubwa wa Milan akiwa mtoto huko Paris na kufichua ushabiki wake unaendelea hadi leo.

"Huwezi kujua nini kinaweza kutokea," alisema Mbappé akiiambia Sky Italia.

"Nilipokuwa mtoto nilikuwa shabiki wa Milan. Siku zote nilisema kwamba ikiwa nitakuja Italia siku moja, nitaenda kuichezea Milan. Huwa natazama ligi ya Italia, kila mechi ya Milan.

"Nilikuwa Paris. Nitakuwa na klabu mpya sasa. Nina furaha sana na nilichonacho kwa sasa."

Mbappé alicheza mechi yake ya mwisho PSG baada ya miaka saba katika klabu hiyo katika ushindi wa mabao 2-1 Jumamosi dhidi ya Lyon kwenye fainali ya Kombe la Ufaransa.

"Nina ndoto nyingi, kushinda kila kombe linalowezekana," alisema. "Lakini sasa, kwa uzoefu, ni zaidi ya kutoa hisia kwa watu wote wanaonitazama, ambao wamenifuatilia tangu nikiwa kijana nataka wawe na hisia wanayosema wanaponitazama nikicheza, 'sawa, tulifurahia kumtazama Kylian akicheza.' Hilo ndilo lengo langu sasa."

Fursa nyingine ya Mbappé ya kushinda medali itakuja na Ufaransa kwenye michuano ya Ulaya msimu huu nchini Ujerumani, ambapo alisema "ana njaa" ya kuongeza medali zake kimataifa.

Mbappé tayari amenyanyua Kombe la Dunia la 2018 akiwa na Ufaransa na kufunga 'hat trick' kwenye fainali ya Kombe la Dunia 2022 lakini akapoteza kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Argentina.

Ufaransa ilitolewa katika hatua ya 16 bora kwenye Euro 2020, lakini Les Bleus ni miongoni mwa timu zinazopewa nafasi zaidi msimu huu wa majira ya joto.




## Raeal Madrid yaweka kikomo bei ya Davies

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid wameripotiwa kujiwekea kikomo cha bei linapokuja suala la kumsajili beki wa kushoto wa Bayern Munich, Alphonso Davies msimu huu wa majira ya joto.

Davies amekuwa akilengwa kwa muda mrefu na Madrid na ataingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Bayern msimu ujao, akiweka kikomo kile ambacho wababe hao wa Ujerumani wanaweza kumpatia kwa njia ya ada ya uhamisho.

Lakini tishio la yeye kuondoka kama mchezaji huru ifikapo mwaka 2025 linaweza kulazimisha kuuzwa ikiwa hakuna makubaliano mapya yatakubaliwa.

Davies na Bayern wanaaminika kuwa hawakuwa na mvutano kuhusiana na mazungumzo ya mkataba mpya, huku mchezaji huyo akitafuta mshahara unaolingana na hadhi yake kama mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani katika nafasi yake.

Klabu hiyo imetoa ofa yao, ambayo ni pungufu ya kile kambi ya Davies iliomba.

Relevo limeandika kwamba mpango wao ni kumsajili Davies kwa muda mfupi iwezekanavyo, akifaidisha hali ambayo imetokea hadi sasa, na bei inayowezekana ya euro milioni 30 hadi 35.

Hiyo ni chini zaidi kutoka kwa makadirio ya awali ya euro milioni 40.





## *Kesi uzembe kifo cha Maradona Oktoba mosi*

**BUENOS AIRES,** Argentina

MAHAKAMA ya ya jinai nchini Argentina imeahirisha hadi Oktoba 1 kuanza kwa kesi ya uzembe wa jinai iliyofikishwa dhidi ya watu nane wanaodaiwa kuhusika katika kifo cha gwiji wa soka Diego Maradona.

Kesi hiyo ilipangwa kuanza kusikilizwa Juni 4, lakini mahakama ya jinai huko San Isidro, nje kidogo ya jiji la Buenos Aires, ilisema katika uamuzi uliochapishwa na vyombo vya habari Jumanne usiku kwamba "maswali kadhaa yameulizwa" na sehemu zote zinazohusika na mauaji hayo.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia la mwaka 1986 alifariki akiwa na umri wa miaka 60 Novemba 25, 2020 kutokana na mshtuko wa moyo.

Uchunguzi ulianza kwa ombi la wanafamilia wa Maradona siku chache baada ya kifo chake.

Watu nane waliofikishwa mahakamani, wakiwemo madaktari na wauguzi, wanadaiwa kuhusika na kifo cha mwanasoka huyo nguli, aliyekuwa akitibiwa katika nyumba binafsi baada ya kufanyiwa upasuaji wa kutoa damu kwenye ubongo wake.

Washtakiwa wamekanusha ukiukaji wowote katika matibabu ya Maradona.

Miongoni mwa maswali ambayo bado hayajajibiwa ni iwapo washtakiwa hao watahukumiwa na mahakimu watatu wa mahakama hiyo au na baraza la majaji maarufu kama mmoja wa wauguzi walioshtakiwa alivyoomba.

zaidi ya mashahidi 200 wanatarajiwa kutoa ushahidi wakati wa kesi hiyo, wakiwemo binti wa Maradona na baadhi ya washirika wake wa zamani.

Ripoti ya kimatibabu ilihitimisha kwamba Maradona alikuwa na shida ya moyo na aliteseka kwa hadi saa 12.

Hati hiyo iliongeza kuwa mwanasoka huyo wa zamani hakupata matibabu ya kutosha katika hali yake.

## HABARI MICHEZO

### Simba sc yaanza

INATOKA UKURASA 24

muda wa kufanya tathimni ya kile kilichotokea baada ya msimu wa mashindano kumalizika, lakini ni lazima yafanyike maboresho kwenye kikosi.

"Ni lazima tupate muda wa kufanya tathmini ili kubainisha mapungufu ya msimu uliomalizika, tutapokea taarifa kutoka benchi la ufundi na maeneo yote, halafu baada ya hapo ndiyo tutajua nini tunatakiwa kufanya.

Lakini kwa namna yoyote ile, tutafanya marekebisho yanayohitajika pale tutakapoona kuna mapungufu na panapohitaji kuboreshwa pataboreshwa na hili tutatoa taarifa rasmi baadaye inayohusu mwenendo wa ligi msimu huu na mashindano mengine tuliyoshiriki," alisema Mwenyekiti huyo.

### Yanga, Azam watunishiana

INATOKA UKURASA 24

kwenye mchezo huo wa fainali.

"Tunashukuru tumemaliza Ligi kwenye nafasi yapili japo tuliutaka ubingwa, lakinisasa tuna mchezo mmoja wa kutuwezeshab kufunga msimu na taji, ni mchezo wa fainali ya FA dhidi ya Yanga," alisema Dabo.

Aidha, alisema wanaiheshimu Yanga lakini watafanya kile walichokifanya kwenye mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu walioibuka na ushindi wa mabao 2-1.

Mchezo huo wa fainali awali ulipangwa uchezwe mkoani Manyara lakini Shirikisho la Soka nchini (TFF) lilifanya mabadiliko na kuupeleka mchezo huo Zanzibar kwa kile ilichoeleza uwanja kutokidhi vigezo.

# TPLB YAUSIFU MSIMU 2023/24

**Na Adam Fungamwangwo**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) imesema msimu wa 2023/ 2024 uliomalizika hivi karibuni ulikuwa msimu bora kuwahi kutokea na kuzipongeza klabu zote zilizoshiriki.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu wa bodi hiyo, Almasi Kasongo, amesema mipango yote waliyopanga msimu huu imekwenda kama ilivyotakiwa, huku akiahidi kuandaa msimu ujao bora zaidi ya uliopita.

Kasongo alisema hayo ikiwa ni salaam za shukrani za Bodi hiyo kwa klabu zote na wadau baada ya kumalizika kwa Ligi hiyo.

"Kwetu tunashukuru mipango yetu imeenda kama tulivyotarajia, tulipanga kumaliza Mei 28, imekuwa hivyo, kanuni inasema ligi ianze Agosti na kumalizika Mei, hilo ndiyo lengo kubwa, tunazishukuru klabu kwa sababu pamoja na ratiba kuwa ngumu bado waliitekeleza, kama unakumbuka kuna misimu mitatu au minne tumeshindwa kumaliza ligi mwezi Mei kama kanuni inavyosema kutokana na changamoto mbalimbali za ratiba za mechi za kimataifa, na ugonjwa wa Uviko," alisema Kasongo.

Mbali na klabu, Ofisa Mtendaji huyo aliishukuru serikali kama mdau wa kwanza, Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), wadhamini wote wa Ligi, Wanahabari na mashabiki wa soka kwa kuchangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha Ligi kuendeshwa vizuri ikiwa na mvuto.

> **"Tumesimamia na tumeendesha katika kiwango ambacho watu wengi walikuwa na matarajio nacho.**

Tumekuwa bora, kila msimu tumekuwa tukipanda, tunatarajia msimu ujao tutafanya vizuri zaidi, najivunia timu ya watendaji niliyo nayo na wadau wote," alisema Kasongo.

Ligi ya msimu huu imeshuhudiwa Yanga ikitwaa ubingwa wa Tanzania Bara, ikikata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa pamoja na Azam FC, iliyomaliza nafasi ya pili huku Simba ikimaliza nafasi ya tatu, Coastal Union ikishika nafasi ya nne na zote kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Kimataifa.

Pia, imeshuhudia Mtibwa Sugar na Geita Gold zikishuka daraja, JKT Tanzania na Tabora United zikimaliza kwenye nafasi ambayo zinatakiwa kwenda kucheza mechi za mchujo 'Play Off'.




Mchezaji mpya wa Azam FC, Jhonier Blanco (katikati) akisaini mkataba wa kuichezea timu hiyo, kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo Abdulkarim Amin 'Popat'. **PICHA: BINZUBERY**

# *Kagera Sugar kukisuka upya kikosi chake*

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la timu ya Kagera Sugar limesema litafanya usajili wa kishindo kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fred Felix 'Minziro' alisema malengo yake ni kuwa na kikosi chenye ushindani msimu ujao ili aweze kushika nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi hiyo.

"Malengo yangu ni kuongeza wachezaji wenye uwezo mkubwa ili tuendeleze ushindani wetu katika msimu ujao ambao naamini utakuwa bora zaidi, alisema Minziro.

Aidha, Minziro alisema msimu uliopita ulikuwa mgumu kwao na wenye ushindani kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu kuhakikisha haishuki daraja.

"Msimu uliopita nilibaini mapungufu ndani ya timu yangu ambayo nitayafanyia marekebisho ili yasijirudie katika msimu ujao," alisema Minziro.

Pia aliwashukuru mashabiki na wapenzi wa timu hiyo kutokana na ushirikiano waliowaonyesha katika kipindi chote cha ligi licha ya kutofanya vizuri kwenye baadhi ya michezo yao.

Timu hiyo imemaliza ligi ikiwa nafasi ya 13 ikiwa na pointi 32 na hivyo kusalia kwenye Ligi hiyo msimu ujao.

# Wasanii watoa msaada gerezani

**Na Judith Julius,** Ngara

SHIRIKISHO la Wasanii wa Wilaya ya Ngara limetoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa wafungwa wa kike waliopo katika gereza la Wilaya hiyo.

Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Oswald Madandi, alisema ofisi yake iliandaa shughuli iitwayo 'Prison Women's Charity' ikilenga kutoa misaada kwa wanawake walioko gerezani.

Vifaa vilivyopelekwa kwa wafungwa hao wa kike ni pamoja na taulo za kike, nyembe, dawa za meno, sabuni, na mafuta ya kupaka.

Madandi msaada huo ulikabidhiwa kwa Mkuu wa gereza hilo Philemon Mduda, mbele ya Afisa tarafa wa Nyamiaga Jawadu Yusuph.

Afisa tarafa huyo alitoa shukrani za pekee kwa Mkuu wa Gereza kwa kukubali kupokea vifaa hivyo ili viwafikie walengwa.

Aidha, aliomba wadau na makundi mengine ya kijamii kuunga mkono shughuli za vijana ili waendelee kuwasaidia watu wengine wengi wenye uhitaji.

Mmoja wa wasanii wa Shirikisho hilo, Justina Charles, alisema wamefanya hivyo ili kugusa maisha ya wanawake walioko gerezani wakiamini kuwa yote wanayoyapitia huko gerezani hata wenzao walioko uraiani wanayapitia.

Msanii huyo vilevile aliwaomba wadau watakaoguswa na jambo hilo wasizuiwe na mtu yeyote kutoa misaada kwa wafungwa wa kike na watu wengine wenye uhitaji.

miongoni mwa wasanii waliokuwepo kwenye tukio hilo, aliwasihi wananchi waishio wilayani humo kuwa na upendo.

**Michezo**

IJumaa Mei 31, 2024


Nipashe



**'Natamani kuichezea AC Milan'** UKURASA 22




Pa Jobe




Freddy Michael

# SIMBA SC YAANZA KUPITISHA PANGA

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Nyota saba wakalia kuti kavu, wawili kuuzwa, lengo ni kuirudisha...

KLABU ya Simba imeanza mipango ya kukisuka upya kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao na mashindano ya Kimataifa huku ikielezwa tayari wachezaji saba tayari wameshaonyeshwa mlango wa kutokea.

**Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema wachezaji ambao tayari wamepigwa panga na wataachwa ndani ya timu hiyo wameshajulikana na watawapisha wachezaji wapya wenye uwezo wa kurudishia makali yake timu hiyo.**

Wachezaji ambao wanaotajwa kuachwa na timu hiyo ni Saidi Ntibazonkiza, Luis Miquissone, Jobe Pa Omar, Freddy Michael, Babacar Sarr, Henock Inonga na mzawa Aishi Manula.



Murtaza Mangungu

Hata hivyo, chanzo cha kuaminika kutoka ndani ya timu hiyo kinasema hilo ni panga la awamu ya kwanza, lakini pia kuna panga lingine ambalo litawahusisha zaidi wachezaji wazawa.

"Vikao vinaendelea kufanya tathimini lakini hao ndi wala ambao ni uhakika watakondoka ndani ya timu, uongozi unaendelea na vikao kuangalia wengine ambao mchango wao haukuwa mkubwa ndani ya timu, lengo ni kubaki na wachezaji ambao walikuwa na mchango na kuwaongeza ambao watakuja kuiinua timu na kuirudisha kwenye nafasi yake msimu ujao," kilisema chanzo hicho.

Kati ya wachezaji hao wanaotarajiwa kuachwa kwa mujibu wa chanzo chetu, Jobe, Freddy na Babacar, wote walisajiliwa kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo msimu uliomalizika, lakini hadi sasa hawajawavutia mashabiki wa klabu hiyo.

Inonga na Miquissone wenyewe wanatarajiwa kuuzwa, huku Manula akimaliza mkataba wake msimu huu na klabu haijaonyesha nia ya kuendelea naye.

Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Murtaza Mangungu, amesema kwa sasa ni lazima wapate

INAENDELEA UKURASA 23

## Yanga, Azam watunishiana vifua

**Na Faustine Feliciane**

ZIKIWA zimebaki siku mbili kabla ya mchezo wa Fainali ya kombe la Shirikisho (FA) kwenye uwanja wa Amaan Complex, Zanzibar, makocha wa Yanga na Azam kila mmoja amejinasibu kwenda kufuata kombe hilo.

Timu hizo zitaumana jumapili kwenye uwanja huo ikiwa ni fainali ya pili mfululizo kukutana katika kipindi cha miaka miwili.

Akizungumza na Nipashe, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi (pichani), alikiri mchezo huo hautakuwa mwepesi lakini ni lazima watimize malengo yao ya kuutetea ubingwa huo.

Alisema anatarajia mchezo wa upinzani lakini anafarijika na molari ya wachezaji wake kuelekea kwenye mchezo huo.

"Ninachoweza kusema hautakuwa mchezo mwepesi, ni lazima tuwe makini, lakini nawaamini wachezaji wangu watanipa kile ninachokitaka, tunataka kutetea na ubingwa huu kama tulivyofanya kwenye Ligi Kuu," alisema Gamondi.

Alisema wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo na kuwaomba mashabiki kwenda kwenda kuwapa hamasa ili kutimiza malengo yao.

Kocha msaidizi wa Azam FC, Youssouph Dabo, alisema wanataka kufunga msimu kwa kuwa na ubingwa hivyo watahakikisha wanapata matokeo mazuri




INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >